Jumapili Machi 3, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581604

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**Mzee** Mwinyi ni chuo halisi cha uongozi

UKURASA 4



**Mwanafunzi** ang'atwa na nyoka akilima shambani kwa mwalimu wake

UKURASA 8



**MAISHA YALIVYO:** Mke alikwenda kusalimia ndugu wakamzuia kurudi

UKURASA 11

# MWISHO WA SAFARI

• **Maelfu** wamzika Mzee Rukhsa Unguja, Samia: maktaba yangu imeungua, familia yatoa siri nzito... *Uk. 2, 3 & 7*



Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakiomba dua wakati wakitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye Mwili wa Rais mstaafu, Hayati Ali Hassan Mwinyi, katika Uwanja wa Amani, Zanzibar jana. **Picha ndogo:** Dk. Mwinyi akiweka udongo kwenye kaburi la baba yake wakati wa maziko katika kijiji cha Mangapwani, Kaskazini Unguja. **Picha zaidi uk. 17. PICHA: IKULU**

# NHIF, hospitali binafsi mambo safi

UK. 5

**MICHEZO** YANGA YAZIPIGIA HESABU POINTI 12 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6






Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa kuaga Mwili wa Rais mstaafu wa Hayati Ali Hassan Mwinyi katika Uwanja wa Amani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwisho wa safari ya Mzee Rukhsa

**Na Waandishi Wetu,** ZANZIBAR

KWAHERI Nzasa, kwaheri Mzee Rukhsa! Saa 12:06 jioni, mlio wa mzinga wa mwisho wa 21 uliopigwa, ulisikika eneo la Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja kuashiria mwisho wa safari ya maisha ya duniani ya Alhaji Ali Hassan Mwinyi.

Maelfu ya wananchi walijitokeza jana kuaga na baadaye kuzika mwili wa Rais huyo wa awamu ya pili ambaye kifo chake kilitangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan Februari 29, mwaka huu.

Kwa jana kuanzia asubuhi hadi jioni, shughuli kubwa katika Kisiwa cha Unguja ilikuwa mazishi ya mwili wa Mzee Mwinyi, maarufu Mzee Rukhsa japo baba yake mzazi, Hassan Mwinyi, alimpa jina la Nzasa alipozaliwa wilayani Mkuranga, mkoani Pwani Mei 8, 1925, miaka 98 iliyopita.

Mwili wa Mzee Rukhsa ulitolewa nyumbani kwake Weleo, Wilaya ya Magharibi B Unguja saa tatu asubuhi, ukipitishwa barabara zinazopita mitaa ya Dimani, Kombeni, Kisauni, Mombasa, Mazizini, Migombani, Kilimani, Mwembeladu hadi Uwanja wa Amani ulikokuwa unasubiriwa na wananchi waliojitokeza kwa ajili ya kuuaga.

Msafara uliokuwa umebeba mwili huo kutoka nyumbani ulikuwa na magari zaidi ya 30 yaliyoongozwa na gari la polisi la kusafisha njia likifuatiwa na gari la Jeshi la Wananchi na pikipiki nne za polisi zilizokaa pande mbili zikiongoza magari hayo.

Licha ya kuwapo mvua na manyunyu katika baadhi ya maeneo, wananchi walionekana barabarani wakinyeshewa mvua wakishuhudia msafara huo.

Wakati mwili huo ukipitishwa barabarani, magari mengine yalizuiwa, hivyo shughuli za usafirishaji kusitishwa kwa muda katika barabara kuu za Uguja. Magari yasiyohusika kwenye msafara huo yaliegeshwa pembeni mwa barabara.

Katika eneo la Kibandamaiti, idadi ya watu iliongezeka, wakisimama pembeni mwa barabara kutoa heshima zao za mwisho, wengi wakinyoosha mikono kutoa ishara ya 'kwaheri'.

Mwili wa Hayati Mzee Mwinyi uliwasili kwenye Uwanja wa Amani saa 4:16 asubuhi, rangi nyeupe na nyeusi zikitawala mavazi ya waliokuwamo uwanjani kuashiria maombolezo.

Mwili huo ulipokewa na kushushwa na maofisa wa juu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kuongozwa na gwaride la kijeshi kupeleka mwili huo katika eneo maalum kwa ajili ya shughuli kuagwa.

Nyuma ya maofisa hao waliobeba mwili wa Mzee Mwinyi, ilikuwapo familia yake. iliyoongozwa na wajane, Mama Siti Mwinyi na Mama Khadija.

Saa 4:25 asubuhi baada ya mwili kuwekwa eneo maalum la kuagwa, shughuli ilianza rasmi kwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar, Wimbo wa Taifa wa Tanzania na Wimbo wa Afrika Mashariki kupigwa kishwa kufuatwa na salama kutoka kwa viongozi mbalimbali wakiwamo wa kiserikali, kidini, wawakilishi wa nchi jirani, wanafamilia, Marais wa Zanzibar wastaafu na Rais Samia Suluhu Hassan aliyehitimisha.

**MSIKITINI MAZIZINI**

Baada ya viongozi mbalimbali kumaliza kuaga mwili na kutoa heshima zao za mwisho kwa Hayati Mzee Mwinyi, wananchi nao walipewa fursa ya kutoa heshima zao kwa mwili wa kiongozi wao huyo.

Ili kupunguza msongamano wa magari kuelekea Msikiti wa Zinjbar Mazizini kwa ajili ya dua na baadaye makaburini Mangapwani, mawaziri na makatibu wakuu wote walitakiwa kutokutumia magari yao, bali mabasi madogo yaliyoandaliwa kwa ajili yao.

Mwili wa Hayati Ally Hassan Mwinyi ulitolewa Uwanja wa Amani saa 7:39 mchana huku mvua kubwa ikinyesha muda mfupi baada ya zoezi la kuagwa kufungwa.

Mwili uliwasili mskitini Mazizini saa 7:57 mchana na kushushwa na maofisa wa vyeo vya juu wa JWTZ kisha kukabidhiwa kwa waamini wa dini ya Kiislamu kwa ajili ya taratibu za ibada ya mwisho.

Saa 8:10 mchana mamia ya waamini wa dini hiyo walikuwa tayari katika msikiti huo wakiendelea na sala ya maiti iliyoongozwa na Mufti wa Zanzibar, Shekhe Swaleh Omar Kabi.

Shekhe Kabi alimtaja Hayati Mzee Mwinyi ni mwanazuoni, hivyo kwa dini hiyo wamepata hasara kubwa kwa kumpoteza mwanazuoni aliyekuwa hazina kubwa kwao.

Baada ya sala hiyuo, saa 8:42 taratibu za kutoa mwili msikitini zilianza, ukikabidhiwa kwa JWTZ kwa ajili ya kuendelea na utaratibu wa kiserikali kuzika kijijini Mangapwani.

Ulipofikishwa Mangapwani, saa 10;00 jioni, mwili wa Mzee Rukhsa uliswaliwa tena sala ya maiti katika eneo maalum lililoandaliwa takriban mita 400 kutoka likokuwa kaburi lake.

Baadaye Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliongoza viongozi na wananchi kuweka udongo katika kaburi hilo. Eneo hilo ndipo alipozikwa mtoto wake mkubwa, Hassan.

Koleo la mwisho la udongo juu ya kaburi la Hayati Mzee Mwinyi liliwekwa saa 11:47 jioni ikiwa ni ishara na kumbukumbu ya mwisho katika safari ya maisha yake duniani.

Dua maalum iliyosomwa mbele ya kaburi lake, ikihitimishwa saa 11:52 ikifuatiwa na dua ya jumla kwa ajili yake pamoja na wanawe iliyoisha saa 11:55 kisha zilifuata taratibu za kiserkali zilizohusisha kupigwa mizinga ya heshima 21, shughuli iliyoongozwa na JWTZ hadi saa 12:06, mzinga wa mwisho ulipopigwa na kufikia tamati ya maziko hayo.

***Imeandaliwa na Sanula Athanas na Rahma Suleiman**

## Rais Samia: Maktaba yangu imeungua moto

**Na Waandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kifo cha Rais wa Pili wa Tanzania, Alhaji Ali Hassan Mwinyi ni pigo kwake binafsi na taifa kutokana na mambo makubwa aliyofanya kiongozi huyo kitaifa na kimataifa.

Amesema kifo cha Rais Mwinyi, maarufu Mzee Rukhsa, ni sawa na kuungua moto kwa maktaba kubwa iliyosheheni vitabu vya maarifa.

"Kifo chake ni pigo kwa taifa na kwangu binafsi kama Mkuu wa Nchi. Nimeukumbuka msemo wa kiafrika unaosema 'anapofariki mzee, maktaba huungua moto', yaani kila kitu alichonacho mzee, akifariki dunia ni kama maktaba iliyoungua moto. Kumbukumbu zote zinapotea," Rais Samia alisema katika salamu zake wakati akiongoza wananchi kuaga mwili wa Mzee Rukhsa kwenye Uwanja wa Amani, Unguja jana.

"Mtakubaliana nami kwamba maktaba yetu kubwa iliyosheheni hadithi nyingi nzuri imeungua moto. Mzee Mwinyi alikuwa maktaba inayotembea iliyosheheni vitabu vyenye mafunzo mengi ya uadilifu, uzalendo, ustahimilivu, ujasiri, unyenyekevu, uchamungu na mambo mengi mengine.

"Msiba huu ni wetu sote, ni msiba wa taifa, ila ni msiba mzito zaidi kwa familia kwa kuondokewa na nguzo yao.

"Mbuyu umeanguka. Kwa niaba ya wananchi wa Tanzania, ninatoa pole kwa familia, ninatoa pole kwa Mama Sitti, Mama Khadija, watoto wa marehemu wakiongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wajukuu na vitukuu kwa kuondokewa na mpendwa wao. Tambueni kuwa pigo hili ni letu sote," alisema.

Rais Samia alisema nchi imepoteza kiongozi mwenye historia kubwa kitaifa, Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla, akimtaja alipenda nchi yake na aliitumikia kwa moyo na kuivusha katika kipindi kigumu kuanzia alipokuwa Rais wa Zanzibar na baadaye Rais wa Tanzania (1985-1995).

"Ingawa tuna simanzi kwa kuondokewa na mzee wetu, tuna faraja kwamba tumemuenzi na kumpa maziko ya kitaifa na kumwombea dua njema," Rais Samia alitia moyo waombolezaji.

Alisema Mzee Mwinyi alikuwa mcha Mungu aliyeishi maagizo ya Mwenyezi Mungu na alitii miongozo ya Dini ya Kiislamu, akiwashukuru wananchi na viongozi wa dini kwa kuungana na serikali kuomboleza kifo cha kiongozi huyo.

Rais Samia pia alishukuru wakuu wa nchi jirani na rafiki waliotuma wawakilishi kushiriki mazishi hayo.

Nchi zilizotuma wawakilishi wake Zanzibar kushiriki mazishi hayo ni Burundi, Namibia na Comoro.

Rais Samia alisema Mzee Mwinyi alipitia kipindi kigumu katika uongozi wake kwa kuwa alichukua 'kijiti' toka kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere ikiwa katika hali mbaya kiuchumi, lakini alihakikisha nchi na wananchi wanakuwa na utulivu.

Alisema kuwa kipindi hicho kulikuwa na uhaba wa fedha za kigeni na bidhaa muhimu, Mzee Mwinyi akibadili sera na kutoa rukhsa ya biashara huria nchini.

Rais Samia pia alimtaja Mzee Rukhsa ni kiongozi wa mfano katika kupenda haki na kutenda haki. Jambo ambalo Rais Mwinyi amelisisitiza katika wosia wake kwa viongozi uliomo katika sura ya mwisho ya kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu'. Rais Samia alimtaja Mzee Rukhsa alikuwa mpenda demokrasia, akiruhusu kusikika sauti tofauti na zilizozoeleka kusikika serikalini, pia vyombo vya habari vya watu binafsi na taasisi ambazo ziliikosoa serikali.

"Mzee Mwinyi ndiye aliyeruhusu uwekezaji binafsi, zikiwamo kampuni za simu. Alama zake zimeendelea kufuatwa na serikali zilizofuata.

Mzee Mkapa, kwa mfano alipata pa kuanzia kuomba IMF kuifutia madeni Tanzania," alisema.

**ALICHOCHOTA**

Rais Samia, akiorodhesha mambo muhimu aliyojifunza kutokana na maisha na uongozi wa Mzee Mwinyi, amtaja alikuwa mwanageuzi asiyeyumba.



## Walichokisema wawakilishi wa wakuu wa nchi jirani

**Na Waandishi Wetu,** ZANZIBAR

NCHI za jirani za Burundi, Comoro na Namibia zimetuma wawakilishi kushiriki mazishi ya mwili wa Ali Hassan Mwinyi.

Katika kuaga mwili huo kwenye Uwanja wa Amani, mjini Unguja jana, wawakilishi wa nchi hizo kwa nyakati tofauti walisema msiba huo si wa watanzania peke yao, bali pia umegusa nchi zao kwa kuwa wanathamini mchango wa kiongozi huyo.

Comoro iliwakilishwa na Waziri wa Kilimo, Uvuvi, Utalii na Mazingira, Houmed Msaidie, aliyesema raia wa Comoro wako pamoja katika msiba huo na wanaikumbuka falsafa ya Mzee Mwinyi - rukhsa.

Alisema kuwa Mzee Mwinyi hakwenda Comoro wakati wa uongozi wake, lakini mwaka 2018 alitembelea nchi hiyo na kuzungumza na wananchi wake na kwamba falsafa yake ya 'rukhsa' wanaijua sana katika kukuza uchumi.

Spika wa Bunge la Burundi, Emmanuel Gagera, alisema Burundi wanaungana pamoja na watanzania katika msiba huo mzito na wanathamini mchango wa Mzee Mwinyi katika kudumisha umoja Afrika Mashariki.

Makamu wa Rais wa Namibia, Netumbo Ndeitwah aliyemwalikisha Rais wa nchi hiyo alisema: "Ukisikia rafiki ana sherehe unampongeza hata ukiwa mbali. Lakini ukisikia rafiki ana msiba, huwezi kulia naye ukiwa mbali, unakwenda kuungana naye kuomboleza.

"Nimekuja hapa (Zanzibar) kuungana na nanyi katika kuomboleza msiba huu mzito, nikimwakilisha Rais na wananchi wa Namibia. Tunatambua mchango mkubwa wa Mzee Mwinyi katika kukuza uchumi na Tanzania na nchi marafiki.

**VIONGOZI WAANDAMIZI**

Katika salamu zake, Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume alisema kamwe hatosahau wosia aliopewa na Mzee Mwinyi mwaka 2000 wakati wa ufunguzi wa kampeni za Uchaguzi Mkuu, kipindi hicho akigombea urais wa Zanzibar.

Dk. Karume aliutaja ni wosia aliopewa na Mzee Mwinyi wakiwa katika viwanja vya Gombani, Pemba wakati akimtambulisha kuwa mgombea. Alimwambia kuwa anaweza kusuluhisha nyoyo za wazanzibari.

"Wakati ananinadi aliuambia umma kuwa 'huyu kijana mimi ninamjua, ana uwezo na atafanya kazi ya kusuluhisha nyoyo za wazanzibari'. Sasa neno hilo liliingia katika moyo wangu na hadi leo ninalo," alisema.

Aliwataka viongozi waliopo madarakani kutousahau wosia huo na kazi ya kusuluhisha nyoyo za wazanzibari iendelee ili kupata amani na utulivu. Dk. Karume alisema wananchi wanazika mwili wa Mzee Mwinyi, lakini hekima na busara zake zitabaki katika mioyo yao.

Rais mstaafu wa awamu ya saba Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema jitihada za Mzee Mwinyi katika kuijenga nchi ni kubwa katika kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Alisema wakati akiwa Rais wa Zanzibar, Mzee Mwinyi alimshauri kuanzisha taasisi ya Siti binti Sadi ili kumwenzi na kuthamini kazi za msanii huyo wa muziki wa taarabu asilia ya visiwani Zanzibar.

Alisema alipokea ushauri huo na kuanzisha taasisi hiyo, akidokeza pia kwamba Mzee Mwinyi alimshauri kuanzisha chuo kikuu katika Kijiji cha Dole visiwani hapa, lakini mpango huo bado haujatekelezwa licha ya eneo la ujenzi kutengwa.



Wajane wa Hayati Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, Mama Siti Mwinyi (wa pili kushoto) na Mama Khadija Mwinyi wakiwasili katika Uwanja wa Amani, mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya kuaga mwili wa mume wao. **PICHA: IKULU**

# Mtoto wake asema hawakuwahi kumwona baba yao akiumwa

**Na Waandishi Wetu,** ZANZIBAR

ABDULLAH Mwinyi, mtoto wa Rais wa awamu ya pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi, amesema hawakuwahi kumwona baba yao akiumwa kabla ya miaka miwili iliyopita alipoanza kuugua maradhi ya saratani ya mapafu yaliyosababisha kifo chake.

Vilevile, amesema kuwa hawakuwahi kumwona baba yao akilia, bali wameshuhudia hali hiyo Rais Samia alipomtembelea kwa mara ya mwisho kabla ya umauti haujamfika.

Abdullah aliyasema hayo jana alipotoa salamu za familia katika kuaga mwili wa Mzee Mwinyi kwenye Uwanja vya Amani, mjini Unguja.

"Sisi watoto hatukuwahi kuona baba yetu (Alhaji Ali Hassan Mwinyi) akiumwa. Tumemwona kwa mara ya kwanza alipoanza kuugua miaka miwili iliyopita.

"Pia hatukuwahi kumwona baba yetu analia. Mheshimiwa Rais, mara ya mwisho ulipokuja kumwona, alilia. Ilikuwa mara yetu ya kwanza kumwona akilia..." alisema Abdullah huku akishindwa kuzuia machozi na kujikuta akihamia kwenye kilio.

Huku akikatisha uwasilishaji salamu za familia mara kadhaa, akilazimika kufuta machozi, Abdullah ambaye ni Msemaji wa Familia katika msiba huo wa kitaifa, alisema wanashukuru Mungu kutokana na mzee wao kuishi miaka 98, umri ambao aliutaja si rahisi kuufikia ukiwa na afya nzuri kama alivyokuwa baba yao.

Mtoto huyo wa marehemu alisema baba yao katika uhai wake alikuwa mtu mwenye utu na aliwaongoza katika misingi mizuri.

Alisema alikuwa na uongozi wa haki, mkweli, jasiri na mwanademokrasia wa kweli.

Abdullah alisema Mzee Mwinyi alikuwa hatishwi na maoni mbadala na ya kwake, alipokea maoni ya kila mtu na kuyasikiliza.

"Kwa kweli hilo ni somo kubwa hasa katika kipindi hiki, tuyapokee maoni mbadala na utofauti wetu, isiwe chanzo cha kufarakana," alisema.

Alishukuru serikali zote mbili pamoja na wananchi kwa kazi kubwa ya kumsitiri mzazi wao pamoja na madaktari waliokuwa wanampatia matibabu kwa uangalizi mkubwa.

Akisoma wasifu wa Mzee Mwinyi, Katibu Mkuu - Utumishi, Juma Mkomi, alisema Rais huyo wa awamu ya pili alizaliwa Mei 8, 1925 wilayani Mkuranga, mkoani Pwani akiwa ni mtoto wa tatu kati ya watoto 10 wa familia ya Mzee Hassan Mwinyi.

Mkomi alisema kuwa Mzee Mwinyi alipata elimu ya malezi na makuzi ya dini ya Kiislamu na alisoma Shule ya Msingi Mangapwani, Zanzibar mwaka 1933 hadi 1936 na ni miongoni mwa wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya kati Shule ya Dole mwaka 1937 hadi 1940 visiwani hapa.

Alisema kuwa Mzee Mwinyi alijiunga na masomo ya ualimu katika Chuo cha Ualimu Dole mnamo mwaka 1941 hadi 1944 na kuwa mwalimu Shule ya Msingi Mangapwani katika ajira yake ya kwanza serikalini.

Alisema Mzee Mwinyi pia alipata mafunzo mbalimbali Uingereza mwaka 1959 na kutunukiwa stashahada ya ualimu.

Alisema baada ya kuhitimu mafunzo hayo alipata cheo na kuwa Mkuu wa Chuo cha Ualimu Dole.

Kuhusu siasa, Mkomi alisema kuwa mwaka 1957, Mzee Mwinyi alijiunga na Chama cha Afroshirazi Party (ASP) kama mwanachama mwazilishi na uanachama wake ulikuwa wa siri kwa sababu ni kinyume cha sheria kwa wakati huo mtumishi wa serikali kuwa mwanachama wa chama cha siasa.

Kuhusu uongozi, Mkomi alisema kuwa mwaka 1964 baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mzee Mwinyi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Zanzibar na alitumikia nafasi hiyo hadi mwaka 1966 alipohamishiwa katika shirika la kimkakati la Serikali ya Zanzibar ambalo lilihusika na karafuu, zao ambalo lilikuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar kwa wakati huo na hata sasa.

Alisema kuwa mwaka 1970, Mzee Mwinyi alitoka katika utumishi wa serikali na kuingia katika utumishi wa kisiasa, akiteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi mwaka 1972.

Alisema mwaka 1984, Mzee Mwinyi aliteuliwa kuwa Rais wa muda wa Zanzibar kwa muda wa siku 90 kabla ya uchaguzi kufuatia Rais Aboud Jumbe kujiuzulu nafasi ya chama na serikali.

Alisema kuwa kufuatia uchaguzi wa mwaka 1984, Mzee Mwinyi alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, akirejea kuwa kuanzia mwaka 1972 mpaka 1975 alifanya kazi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Naibu Waziri wa Afya chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere.

Mkomi alisema kuwa mwaka 1975, Mzee Mwinyi alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini mwaka 1977 alijiuzulu kwa kuwajibika kutokana na mauaji ya wafungwa mkoani Shinyanga yaliyofanywa na maofisa katika wizara yake na uwajibikaji wake huo ulimpatia heshima kubwa.

Alisema kuwa mwaka 1978, Mzee Mwinyi aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Misri na mwaka 1981, aliteuliwa kuwa Waziri wa Utalii na Maliasili na mwaka 1985 alichaguliwa kuwa Rais wa Tanzania.

Akitoa salamu za Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Mkuu wa Mkoa huo, Idrisa Kitwana Mustafa alisema Mzee Mwinyi ni mwanamageuzi na kizazi cha sasa kinapaswa kujifunza mambo mema na mazuri aliyoyafanya.

"Tutaendelea kujifunza siku zote kwa matendo mema ya mzee huyu kwa wema wake, busara, unyenyekevu, heshima, utulivu na uvumilivu," alisema Kitwana.

Kifo cha Mzee Mwinyi kilitangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan Februari 29, mwaka huu. Mkuu wa Nchi pia alitangaza siku saba za maombolezo kitaifa kuanzia Machi Mosi mwaka huu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI ARUSHA**
**MADAI NAMBA 1/2024**
**MUKHTAR AKBARALI GULAMHUSSEIN..........MDAI**
**DHIDI**
**SILAS IBRAHIM @ MOLLEL............MDAIWA WA KWANZA**
**BIRTHAVEN SIMBO MUSHI ...........MDAIWA WA PILI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA SILAS IBRAHIM @ MOLLEL**
**ARUSHA**
**TANZANIA**

**POPOTE ULIPO**
**MUKHTAR AKBARALI GULAMHUSSEIN.** Amewasilisha shauri la madai namba 1 ya mwaka 2024 mbele ya mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha , Shauri la madai hayo yamepangwa kutajwa tarehe 4/3/2024 saa mbili na nusu asubuhi . Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria bila kukosa. Endapo hauta hudhuria , hadai haya yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/Amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa Muhuri na Mahakama ya hakimu Mkazi tarehe 23/2/2024,

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
ARUSHA.
RESIDENT MAGISTRATE
ARUSHA

## BURIANI ALI HASSAN MWINYI



# Mzee Mwinyi ni chuo cha uongozi

## -Unyenyekevu, uvumilivu ndio msingi wa mafanikio

**Na Mwandishi Wetu**



RAIS Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, jana alipumzishwa rasmi kijijini kwao, Mangapwani, kisiwani Unguja baada ya kufariki dunia Februari, 2024 katika Hospitali ya Emilio Mzena, Dar es Salaam. Yako mengi ya kumwelezea kiongozi huyo kutokana na mambo aliyoyafanyia kazi katika uongozi wake. Mwandishi DEREK MURUSURI, ambaye aliwahi kufanya naye kazi, anamwelezea katika Makala yake hii binafsi.

Tulikuwa tunahitimisha ziara ya Rais ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 1993. Tulikuwa kwenye msafara wa Rais Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1985 hadi 1995.

Mara tukaambiwa Mheshimiwa Rais anataka kupiga picha na wapigapicha wake. Lo! sisi? Mbio tukaenda. Akatusalimia kwa kutushika mkono, akitushukuru kama baba kwa mwanawe.

Alifurahia jinsi habari zake na hasa picha, zilivyokuwa zikipigwa na kuchapishwa katika magazeti mbalimbali nchini. Alikuwa mtu wa kushukuru.

Wakati huo nilikuwa mmoja wa wapigapicha au 'photojournalists' kutoka Idara ya Habari - MAELEZO. Bosi wangu, Raphael Hokororo alinipanga kwenye ziara hiyo. Mheshimiwa Rais Mwinyi akatuita: "Njooni tupige picha ya ukumbusho."

Hima tukajongea. Akiwa na mkewe, Mama Sitti Mwinyi, waliketi, sisi wapigapicha tukasimama nyuma yao. Mpigapicha mmoja akatupiga picha sisi wapigapicha pamoja na Rais na mkewe. Baada ya kumalizika upigaji picha huo, akatuaga.

Si viongozi wote wanaojua kushukuru. Fikiria, Rais anakushukuru kwa kutekeleza wajibu wako, tena kiongozi mkuu wa taifa, halafu wewe ni mpigapicha tu.

Mwaka huo huo, nilifanya naye kazi Ikulu kwa wiki mbili na ushee hivi, chini ya Balozi Patrick Chokala. Kipindi hicho, mpiga picha wake, Mzee Henry Isike, alikuwa likizo. Wakubwa wangu pia walikuwa safari. Nilipomwomba asogee hivi ili picha itoke vizuri, alikubali kwa unyenyekevu mkubwa sana.

Nikiwa Tume ya Mipango, iliyokuwa chini ya Ofisi ya Rais, Rais Mwinyi ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume. Nilihudhuria kikao kimoja cha Tume ya Mipango katika chumba cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, nikashuhudia hekima yake kubwa ya kuendesha vikao. Alimsikiliza kila mwenye hoja, tena kwa umakini mkubwa. Ulihitaji kuwa karibu na Rais Ali Hassan Mwinyi, ili umfahamu.

Alikuwa kiongozi mnyenyekevu sana, mvumilivu, mwanamageuzi, aliyeujenga upya uchumi wa Tanzania baada ya kuharibiwa sana na vita vya Kagera na hata vita vya harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika.

Naweza kusema kuwa Mzee Ali Hassan Mwinyi alikuwa Deng Xiaoping wa Tanzania, kwa kipindi kile kuanzia mwaka 1985. Deng ndiye Baba wa Uchumi wa China.

Aliwahi kupigwa kofi katika hafla moja ya kidini pale Diamond Jubilee, Dar es Salaam na kijana mmoja 'bastard' tu hivi. Kwa vile alikuwa anajichanganya na raia, akamsamehe. Alishambuliwa sana kwa maneno mengi hadi familia yake ikashutumiwa, lakini akanyamaza kimya.

Akaendelea kuchapa kazi. Akameza kibri chake, akajishusha. Hakujitutumua, patachimbika, Si yule Baba. Alitoa kombe kwa mahasimu wake, yeye akajielekeza kwenye kazi ya kufanya mageuzi ya uchumi wa Tanzania.

Wakati huo, alikuwa Amiri Jeshi Mkuu. Majeshi ya ulinzi na usalama yalikuwa chini yake. Hata kama mahakama ni mhimili tofauti, angeweza kushawishi ili mahasimu wake waadhibiwe lakini hakuitumia nafasi yake wala maguvu kuwashikisha adabu mahasimu wake.

Alikaa kimya, akasamehe. Tena akafanya kazi na mahasimu wake. Akaondoa foleni za kununua sembe. Sabuni za kufulia na dawa za mswaki zilizokuwa adimu zilizokuwa zinapatikana kwa magendo, zikajaa madukani.

Watu walifulia nguo sabuni za MAGWANJI, wenye bahati ya kuwa na mipapai, wakatumia majani yake kufulia nguo. Mzee Ali Hassan Mwinyi akanyamaza kimya ili aujenge upya uchumi wa taifa la Tanzania. Akachapa kazi. Akawaamini watu. Hakuchukua maguvu yote peke yake. Nchi ikasimama.

Mzee Ali Hassan Mwinyi ni chuo. Yako mengi sana ya kujifunza kutoka kwake hakika. Alikuwa kiongozi makini na alijitoa sana kwenye mambo ya kijamii. 'Power Distance' (umbali wa kimamlaka) kwake ilikuwa kidogo. Yaani, alikuwa karibu na raia aliowaongoza.

Mbali na kufanya mazoezi ya kutembea kila siku, huenda ndiyo siri ya kuishi miaka 98 na miezi 9, takriban miaka 99, alijaliwa na Mola wake kwa kuonyesha maisha ya msamaha. Alifundisha Kiswahi kwa kujitolea nchini Uingereza.

Abdullah Ali Hassan Mwinyi, Mbunge wa zamani wa Afrika Mashariki, ambaye ni mmoja wa watoto wa Mzee Mwinyi, alipata kunieleza tukiwa Chuo Kikuu cha Cardiff kuwa wakati Mzee Mwinyi akiwa Uingereza, alijitolea kufundisha Kiswahili kwa bidii sana.

Ndiyo maana Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na vyombo vya Habari, vilimtumia vizuri hapa nyumbani. Alijua, tukiwa na lugha yetu, ikakua na kutumika hata kwenye sayansi, taifa litapata maendeleo makubwa.

Hili ni somo kubwa sana la unyenyekevu katika uongozi kwa Watanzania na waafrika wote. Si kwa viongozi wa kisiasa pekee bali ni katika maisha ya kila mmoja wetu. Nyumbani, ofisini, katika jamii na taifa.

Hata Nabii Issa Bin Maryam, Bwana Yesu Kristo, alijishusha na kunyenyekea sana. Kuna nyakati alinyamaza pasipo kusema neno lolote. Hakutumia uwezo wake wa kiungu kuwasaga adui zake. Nimeamini, Mwenyezi Mungu huwapenda watu wanyenyekevu, wenye huruma na wacha Mungu.

Basi, ngoja kiongozi wetu, mzee wetu, baba yetu, rafiki yetu, apumzike kwa amani. Mzee wetu Ali Hassan Mwinyi, hakika aliutumia vizuri muda wake hapa duniani. Kumbe humility (ustahimilivu) ni msingi mkuu wa kiongozi bora na namna njema ya kuishi hapa duniani.

Hata alipolazimika kujiuzulu, ilifika mahali yeye na familia yake wakapatiwa hifadhi na rafiki wa karibu. Hakuwa mbadhirifu. Alikuwa mwadilifu. Lakini hakujisikia vibaya. Muda ulipofika, Mwenyezi Mungu akamkumbuka. Alikuwa mvumilivu sana. Huyu kiongozi wetu aliyeondoka, hakika alikuwa binadamu wa pekee sana.

Nilifurahi kumwona, yeye na mke wake, Mama Sitti, wakitumia usafiri wa daladala, mwendokasi. Nilifurahi sana. Hii ni ishara ya unyenyekevu. Hakuzungumzia unyenyekevu bali maisha yake yalitangaza unyenyekevu.

Tena siku hiyo haikutangazwa kwenye vyombo vya habari kuwa Mzee Mwinyi atatumia usafiri wa mwendokasi, alifurahi kusafiri na wananchi wa kawaida aliowaongoza. Alipenda maendeleo.

Alijaliwa kipaji cha hekima kubwa. Kwa kweli ameacha funzo kubwa kwenye kada ya uongozi katika bara la Afrika.

Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi, amjaaliye Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, pumziko la amani hadi tutakapoonana.

**INNA LILLAHI WA INNA ILAYHI RAJIUN**

HABARI KITAIFA

# NHIF, hospitali binafsi sasa mambo safi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO safi. Ndivyo ilivyo baada ya hospitali binafsi zilizotangaza kutowapokea wagonjwa ambao ni wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuanza kutoa huduma.

Hospitali hizo zilitangaza jana kurejeshwa utaratibu huo kwa kile zilichodai kuwa hawakufikia makubaliano na serikali kupitia NHIF kuhusu mabadiliko ya vifurushi vipya vya mfuko huo vilivyotangazwa kuanza kutumika juzi.

Baadhi ya hospitali hizo zilizotangaza uamuzi huo kupitia Chama cha Watoa Huduma Binafsi za Afya Tanzania (APHFTA) ni Aga Khan, Masana, Regency Medical Centre, TMJ, Kairuki na Boch.

Baada ya kutangaza uamuzi huo, serikali kupitia Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ilisema bado kuna nafasi ya mazungumzo kuhusu jambo hilo na kuwataka wadau hao warudi kweye meza ya mazungumzo.

Kutokana na kauli hiyo, hospitali hizo zilitangaza jana kwamba zimerejesha utaratibu wa kuwapokea wanachama wa NHIF baada ya kuwapo mwanga wa kurejewa mazungumzo ili kufikiwa kwa mwafaka katika jambo ambalo lilisababisha kutokea kwa hali hiyo.

Hospitali ya Bochi katika tangazo lake, ilisema imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wote, walioko wodini na chumba cha uangalizi maalumu (ICU) na kwamba huduma za NHIF zimerejea kama kawaida.

Baada ya tangazo hilo, Waziri Ummy katika ukurasa wake wa X (zamani Twitter), aliandika: "Asanteni sana Bochi na wote mliorudisha huduma kwa wanachama wa NHIF. Tunawashukuru sana sana. Ninawaahidi kuwa tutafanya maboresho katika maeneo mahususi mtakayoainisha ndani ya muda mfupi."

Aidha, uongozi wa Hospitali ya Kairuki, ulitangaza kuwa imerejesha huduma kwa wanachama wa NHIF baada ya kutangaza kusitisha kuanzia saa 6:01 juzi, muda rasmi uliotangazwa kuanza kutumika kwa vifurushi vipya vya mfuko huo.

"Taarifa hii (ya kurejeshwa kwa huduma) inakuja kufuatia (kutokana) na mazungumzo yanayoendelea kati ya serikali na APHFTA," ilibainisha taarifa hiyo huku ikiwaomba radhi wagonjwa waliokosa huduma hiyo juzi.

Awali, NHIF katika taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Meneja Uhusiano, Grace Michael, ilisema vituo vilivyokuwa vimesitisha huduma hizo, vimerejesha huduma kama kawaida.

"Vituo hivyo ni Regency Medical Centre, Hospitali ya TJM, Hospitali ya Apollo na Bochi,' ilisema taarifa hiyo huku ikivikumbusha vituo vingine vilivyositisha, ambavyo vina mkataba wa kutoa huduma kwa wanachama wa NHIF, kurejesha mara moja.

**HALI ILIVYOKUWA**

Kutokana na tangazo la hospitali hizo kusitisha huduma kwa wanufaika wa NHIF, Nipashe ilishuhudia katika baadhi ya vituo hivyo wagonjwa wakizuiwa huku waliokuwa na uwezo wakitumia fedha taslimu ili kuepuka usumbufu pamoja na hali za ndugu zao.

Mwananchi mmoja, aliyejitambulisha kwa jina Collins Lema, aliyekuwa amempeleka mama yake mzazi katika hospitali moja (zilizotangaza kusitisha huduma za NHIF), alisema amelazimika kulipa Sh. 250,000 ili kuwezesha mzazi wake, mwenye tatizo la figo, kusafishwa damu.

Uchunguzi wa Nipashe pia ulibaini kuwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) ilikuwa na wagonjwa wengi waliokuwa wakienda hapo baada ya kushindwa kupata huduma kwenye hospitali binafsi zilizotangaza kusitisha huduma.

Pia ilibainika kuwa wagonjwa wengi waliokwenda hapo, wengi walikuwa wenye maradhi sugu kama vile figo, hali ambayo ilisababisha wafanyakazi kufanya kazi za ziada huku kukiwa na foleni kwenye maeneo ya huduma hizo.

**KAULI YA WAZIRI**

Waziri Ummy baada ya kuwapo hali hiyo juzi, aliwaagiza watoa huduma hao kuendelea kutoa huduma na endapo kuna shida katika kitita hicho, warudi katika meza ya majadiliano na serikali badala ya kusitisha huduma.

Ummy alisema gharama za mwisho ambazo zimewekwa katika kitita Januari 4, mwaka huu, alikutana na timu yake ya wataalamu wa wizara ambao walifanya kikao cha pamoja na wadau wa NHIF. Alisema katika kikao hicho walikuwepo wamiliki wa vituo vya afya binafsi, Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC), Kamati ya Afya chini ya Bakwata, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Chama Cha Madaktari Tanzania (MAT) na NHIF kwa lengo la kusikiliza hoja za wadau. Januari 4, mwaka huu, alisema wizara iliamua kusitisha utekelezaji wa kitita kipya cha NHIF cha mwaka 2023 na kuunda kamati yenye wadau kutoka serikalini, sekta binafsi na taasisi za bima kwa ajili ya kuishauri serikali.

"Kwa sababu hakuna vigezo vingine waje mezani watueleze tumewawekea faida ndogo kwa kutueleza dawa wamenunua kwa kiasi gani? na gharama za uendeshaji zipoje? waje waseme kama dawa hii haiuzwi bei fulani sio mseme hatutaki kitita. Leteni hoja zenu mezani. Kamati naipongeza imefanya kazi nzuri," alisema Waziri.

"Nawaomba warudi kwenye meza ya mazungumzo. Kamati imeweka vigezo, waje waseme vigezo hivi havipaswi kutumika katika kutoa huduma za afya," alisisitiza.

Ummy alisema baada ya kupata taarifa ya kamati aliitisha kikao kingine Februari 17 na kuwapatia taarifa hiyo, hakuna hata mmoja aliyesema hawakubaliani na vigezo hivyo.

Waziri Ummy alisema serikali imeielekeza NHIF kuendelea kupokea maoni ya wadau kuhusiana na kitita hicho wakati wa utekelezaji.

Naomba nieleze kumekuwa na ushirikishwaji mkubwa wa wadau katika mchakato huo nimewasikiliza mimi na timu yangu tangu mwaka 2022 tunachelewa lakini tumekuwa wavumilivu milango ya wizara ipo wazi," alisema.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuna mambo mengi ya kujifunza kupitia maisha ya Mzee Mwinyi

**MWANADAMU** huzaliwa, kuishi na kufa. Hiyo ndiyo kweli kuhusu maisha ya mwanadamu ambaye kama maandiko matakatifu yasemavyo, hakika atarejea kwa Mola wake. Pia maandiko yanasema mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi nazo hujaa taabu na mahangaiko.

Maneno hayo yanathibitidha ukweli kwamba mwanadamu baada ya kuzaliwa hukua na kufanya mambo mbalimbali na mwisho wake atarudi mavumbini (atazikwa). Hapo ndipo mwisho wa mwanadamu awe tajiri au maskini, mweupe au mweusi.

Hivyo ndivyo inavyosadifu na maisha ya Rais mstaafu wa awamu ya pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, ambaye safari yake ya maisha duniani ilitamatika jana baada ya kuzikwa kijijini kwao, Mangapwani, kisiwani Unguja. Baada ya kifo chake, mambo mengi yameelezwa juu yake yakiwamo upole, unyenyekevu, uvumilivu, kutokuwa na visasi na kuheshimu watu bila kujali imani, itikadi wala asili yao.

Katika hilo, mzee mwinyi alionyesha kwa vitendo mwaka 1993 baada ya kuibuka vikundi vya dini ya Kiislamu vilivyoendesha mihadhara na kukashfu Ukristo. Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, aliibuka na kukemea huku akisisitiza kila mtu ana uhuru wa kuabudu kulingana na imani na dini yake na asiwapo mtu wa kukashfu imani ya mwingine.

Aidha, vikundi hivyo vilivyokuwa vikikashfu Ukristo, pia vilikashfu watu wanaotumia kitoweo cha nguruwe kuwa ni haramu. Hawakuishia hapo tu bali walivamia na kuvunja bucha zilizokuwa zikiuza nyama hiyo katika maeneo mbalimbali yakiwamo Magomeni na Kigogo, Dar es Salaam. Mzee Mwinyi alisimama na kukemea huku akisema kila mtu anaruhusiwa kufanya anachokiona kinafaaa bila kuingiliwa na mtu mradi havunji sheria. Pia alisema kila mtu rukhsa kula anachotaka hata kama ni mjusi. Hapo ndipo alipopewa jina la Mzee Rukhsa.

Alipoingia madarakani mwaka 1985, Mzee Mwinyi aliikuta nchi ikiwa katika hali mbaya kiuchumi kutokana na pamoja na mambo mengine, vita vya Uganda, hivyo kufanya mageuzi ya kiuchumi. Katika kipindi cha uongozi wake kilichokoma mwaka 1996, alifanya mageuzi katika siasa kwa kuwezesha nchi kuingia katika mfumo wa vyama vingi.

Pia aliruhusu uhuru wa vyombo vya habari na kushuhudiwa magazeti yakianzishwa na vituo vya redio na televisheni kufunguliwa. Kutokana na kuwapo kwa mabadiliko hayo ya kiuchumi, kisiasa na uhuru wa vyombo vya habari, Mzee Mwinyi aliitwa Baba wa Mageuzi. Sambamba na hayo, Mwinyi alithubutu kuvunja Baraza la Mawaziri mwaka 1900 na 1994 hali iliyodhihirisha alivyokuwa mtu jasiri na mwenye uthubutu.

Si hivyo tu, mwaka 1976 alikubali kuwajibika kwa kujiuzulu wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi baada ya kutokea mauaji yaliyotokea mkoani Mwanza licha ya kwamba hakuhusika.


Kutokana na mambo hayo aliyoyafanya, Mwinyi ameacha darasa kubwa kwa Watanzania, si viongozi wala wananchi wa kawaida, juu ya kuishi maisha mema na yenye kumpendeza Mwenyezi Mungu na wanadamu.

Wako watu ambao pindi wanapofanikiwa na kuwa na ukwasi, basi hujiinua na kuwadharau wengine na hata kutumia fedha zao kuwanyanyasa kimwili, kiuchumi na kisaikolojia. Pia wako watu ambao mara wanapopata uongozi, hutumia nafasi zao kujinufaisha na familia zao huku wakiwaacha wananchi waliowapa dhamana na kuteseka na hata kunyanyasika. Watu hao hutumia madaraka yao kuwaumiza wengine ikiwamo kuwafunga au kulipiza visasi kutokana na tofauti walizokuwa nazo kabla hawajawa viongozi.

Kupitia somo aliloliacha Mzee Mwinyi, Watanzania kwa nafasi zao za uongozi au kiuchumi, wanapaswa kuwa na upendo na kuwajali watu wenye uhitaji badala ya kuwanyanyasa na kuwafanyia chuki na fitina. Matendo mema aliyoyafanya Mzee Mwinyi wakati wa uhai wake, yameacha alama kubwa juu yake na yana mfanya aendelee kuishi licha ya kwamba ametangulia mbele za haki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wafanyabiashara wasigeuze sukari kuwa biashara haramu

**MSAKO** dhidi ya wafanyabiashara wanaouza sukari bila kuzingatia bei elekezi ya serikali, unaendelea, huku baadhi yao wakikamatwa lengo likiwa ni kila moja afuate maelekezo ya serikali.

Bei elekezi ya serikali ni kati ya Sh. 2,800 na 3000 kwa kilo moja lakini badala yake baadhi ya wafanyabiashara wanauza kilo moja kati ya Sh. 4000 hadi 5,000, bei ambayo inaumiza watumiaji.

Viongozi wa Bodi ya Sukari Tanzania wanabainisha kuwa licha ya serikali kufuta ushuru wa kuingiza sukari nchini, bado baadhi ya wafanyabiashara wameendelea kukiuka bei elekezi iliyopangwa na serikali.

Kwa mtindo huo, ni wazi kwamba unaweza kusababisha kuendelea kuwapo kwa ugumu wa kupatikana bidhaa hiyo kwa walaji, hivyo, ninadhani ni vyema waendelee kubanwa.

Aidha, katika mazingira hayo ya kutozingatia bei elekezi, sasa baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kuuza sukari kwa bei ya juu, tena kwa kificho kana kwamba ni biashara haramu wakikwepa kukamatwa.

Baadhi yao wanawauzia wateja wanaowafahamu, tena kwa bei isiyo elekezi. Mtu ambaye ni mgeni hawezi kuuziwa, ataambiwa hakuna sukari, kitendo kinachosababisha baadhi ya watu waendelee kuumia.

Sukari si bidhaa haramu, hivyo ingekuwa vyema kama wafanyabiashara watazingatia maagizo ya serikali, wauze kwa bei elekezi, kuwaondolea wananchi kero zisizo za lazima ambazo sasa wanakumbana nazo.

Inawezekana baadhi ya wafanyabiashara walifanya ujanja kwa kununua sukari nyingi na kurundika ndani, wakivizia kwamba siku ikiadimika, wao waiuze kwa bei ya juu wapate faida kubwa.

Kama wako wa aina hiyo, ninadhani hawawatendei haki Watanzania wenzao, bali ninaamini kuwa hadi serikali kuweka bei elekezi, kuna vitu ambavyo imezingatia ikiwamo kila upande kufaidika, si kuumiza.

Lakini badala yake hawashushi bei hadi kwanza ile ambayo walirundika ndani iishe, matokeo yake ni kusumbuana na serikali, huku walaji wakiendelea kuumia kwa kununua kwa bei ya juu au kuikosa.

Si vyema kila mfanyabiashara kuwa na bei yake ya kuanzia Sh. 4,000 hadi 6,000 kwa kilo, huku kukiwa na bei elekezi, ambayo inalenga kutoa unafuu kwa walaji na wafanyabiashara wenyewe.

Serikali imeshatoa maelezo kuhusu kuwapo kwa uhaba wa sukari, kwamba umesababishwa na mvua nyingi inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya nchi na kusabisha viwanda vya sukari kushindwa kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa.

Pamoja na hayo, inaeleza kuwa imechukua hatua mbalimbali za kuwaondolea makali wananchi, kwa kutoa vibali vya kuruhusu uingizaji wa sukari wa takriban tani 100,000 kutoka nje.

Licha ya kuagiza kiasi hicho cha sukari, serikali pia imewaagiza wenye viwanda kusimamia usambazaji wao kama kawaida bila kumuumiza mlaji, hivyo ninadhani maelekezo hayo ni muhimu kuzingatiwa.

Tanzania ina viwanda saba vya sukari, inalezwa kuwa vikubwa kati ya hivyo ni Kilombero, ambacho kwa siku kinazalisha tani 700 za sukari, hata hivyo kiwango kimeshuka hadi 250.

Kwa upande wa TPC, inaelezwa kuwa kwa siku kinazalisha tani 450, lakini kwa sasa kimesimamisha uzalishaji kutokana na hitilafu za mashine, huku Kagera Sugar kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 500 kwa siku, lakini sasa kinazalisha wastani wa tani 200 hadi 300 kwa siku.

Hata hivyo, viwanda vingine vya Mtibwa na Bagamoyo, kwa mujibu wa serikali, uzalishaji wake umepungua hadi kufikia takriban tani 1000 kwa siku, kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Uhaba huo wa sukari na kupungua kwa uzalishaji katika viwanda, visiwe fimbo ya kuumiza walaji kama ambavyo inaendelea sasa wakati serikali ilishatoa bei elekezi ya bidhaa hiyo.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Buriani Mzee Rukhsa, Baba wa demokrasia na uhuru wa habari



Pascal Mayalla

JANA, tulimpumzisha mzee wetu, Rais Mstaafu wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi, maarufu kwa jina la la Mzee Rukhsa, kwenye nyumba yake ya milele.

Kwa mara ya kwanza, jina la Ali Hassan Mwinyi nililisikia mwaka 1977, wakati huo akiwa ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati wa serikali ya awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere. Nililisikia jina hilo alipolazimika kujiuzulu kutokana na kashfa ya vifo vya watuhumiwa wawili wa mauaji ya vikongwe huko Mwanza mwaka 1976.

Mwinyi hakuwa peke yake, bali aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, Rashidi Mfaume Kawawa, pia aliondolewa. Waziri katika Ofisi ya Rais, aliyekuwa anashughulikia Usalama wa Taifa, Peter Siyovelwa naye aliondolewa, akafutiwa na watendaji wakuu wa vyombo vya usalama.

Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Emelio Mzena, akastaafishwa kwa manufaa ya umma, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Samweli Pundugu, naye akastaafishwa kwa manufaa ya umma.

Baada ya Baba wa Taifa kuwafagia wakuu hao, fagio la chuma likatua Mwanza kwa kuondolewa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa, Peter Kisumo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa (RPC) Ofisa Usalama wa Wilaya (RSO), Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) na Ofisa Usalama wa Wilaya (DSO) Mwanza nao wakafutwa kazi.

Wote hao pia walishtakiwa kwenye kesi maarufu ya Mauaji Mwanza ya Mwaka 1976. Mtu pekee aliyesalimika kati ya hao washtakiwa ni Andrew Mayalla na salama yake, mdogo wake anayeitwa Mathew Kasanga, alimweka wakili mahiri Murtaza Lakha, kumtetea kaka yake. Wote walikula mvua za kutosha.

Tukio hilo lilileta mageuzi makubwa nchini, kwanza Idara ya Usalama wa Taifa ilifumuliwa na kusukwa upya kwa kufanyiwa mabadiliko makubwa. Ikaletwa Sheria ya Usalama wa Taifa ya Mwaka 1976, Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976 na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Jina la Ali Hassan Mwinyi nikaja kukutana nalo tena shule ya msingi, tukisoma na mtoto wake, Hussein ambaye alinitangulia madarasa mawili. Baada ya shule ya msingi nikajiunga Shule ya Sekondari ya Tambaza. Ile mwaka 1985 Mzee Mwinyi anakuwa Rais wa Tanzania, yule mtoto wake, Hussein, alikuwa anasoma kidato cha tano mchepuo wa Fizikia, Kemia na Baiolojia (PCB) pale Tambaza. Kitendo cha mtoto wa Rais kusoma shule moja, halikuwa jambo dogo, sasa ndiyo nikazidi kumfahamu Ali Hassan Mwinyi kwa karibu. Wakati huo hapo Tambaza pia tulikuwa na mtoto wa aliyekuwa Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Nyerere, na mtoto wa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, darasa moja.

**KUITWA MZEE RUKHSA**

Wakati Mwinyi anachukua urais mwaka 1985, hali ya uchumi ilikuwa 'dhollfu bin taaban', baada ya vita vya Kagera na Mwalimu Nyerere kutangaza miezi 18 ya kufunga mikanda. Mambo kwa kweli yalikuwa magumu.

Tulikula unga wa njamo, maarufu kama 'Unga wa yanga' kutoka Marekani ambao kule kwao ulikuwa chakula cha mifugo! Watu wamevaa magunia, sandarusi hadi sisi wanafunzi nchi nzima tumevaa sare ya kitambaa maarufu kama madurufu, ambacho ni pamba chafu ya kutupa.

Mahitaji muhimu yote ni kwa mgawo kupitia maduka ya kaya.

Tulikuwa tunapanga foleni siku nzima kusubiri kuuziwa kilo mbili mbili za sukari, hivyo watoto wote mnatumwa. Ili kuwahi foleni, watu walidamka asubuhi na kupanga mawe. Gari linaweza kuja saa 10 jioni au siku nyingine haliji kabisa.

Nchi za mabeberu zilimpa Mwalimu Nyerere masharti magumu ya kutupa misaada, ndipo akaamua kuliko kugeuka nyuma na kuwa jiwe la chumvi, bora aachie ngazi, kwa mtindo wa kung'atuka na kumpisha Mwinyi. Hivyo Mwinyi aliipokea nchi ikiwa kwenye dhiki kubwa.

Baada ya kuingia Rais Mwislamu, kukaibuka vikundi vya Waislamu wa siasa kali. kwanza waligomea nguruwe kuchinjwa mahali pamoja na nyama yake isiuzwe katika bucha zile zile za nyama ya kawaida.

Vikundi hivyo vikaleta vurugu za kulazimisha nyama ya nguruwe ipigwe marufuku kwa sababu ni haramu na kuanzishwa mihadhara ya kashfa. Kwa wanazuoni wa dini hiyo, walianza kuikosoa Biblia na kusema hata katika kitabu hicho, inaelezwa kuwa nguruwe ni haramu.

Vurugu hizo zilisababisha kuvunjwa kwa bucha za nyama ya nguruwe maeneo ya Magomeni na Kigogo, Dar es Salaam na sehemu zingine kisha wahusika kukimbilia kujificha misikitini.

Hatua hiyo ilisababisha Rais Mwinyi kutangaza rukhsa mtu yeyote kula kitu chochote. Hakuna rukhsa ya mtu mwingine yeyote kuingilia uhuru wa mtu wa dini nyingine yoyote kula chochote 'rukhsa'. Huo ukawa mwanzo wa kuitwa Mzee wa Rukhsa.

Wale waliohusika na vurugu hizo kwa kisingizio cha dini walishughulikiwa kikamilifu.

Baada ya kuzifungulia hizo rukhsa, alifungulia rukhsa zingine nyingi za biashara, uchumi, akalipindua Azimio la Arusha lililoweka miiko ya uongozi na kuleta Azimio la Zanzibar ambalo liliruhusu viongozi kufanya biashara na kumiliki mali na hapa sasa ndipo viongozi wa umma wakaanza kuwa matajiri.

Rukhsa nyingine kubwa Rais Mwinyi aliyotuachia ni mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania kiasi kwamba sifa ya Baba wa Demokrasia Tanzania inamstahili kabisa!, Mwinyi ndie Deng Xioping wetu! Si hivyo tu, pia aliruhusu uhuru wa vyombo vya habari Watanzania tukashuhudia kuibuka kwa magazeti mbalimbali na televisheni na redio binafsi wakati wa uongozi wake.

Japo Rais Mstaafu Ali Haasan Mwinyi, Mzee Rukhsa, ametutoka kwa kutangulia mbele ya haki, huku nyuma rukhsa zake tutanzienzi milele.

Buriani Ali Hassan Mwinyi, Mwendo Umeumaliza.

Inna lillahi wa inna ilayhi rajiun

Paskali
Mob. +255 754 270403

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Heri yenu mliohamia Msomera kwa hiari



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MARA nyingi Serikali imekuwa ikifanya mambo kwa ajili ya wananchi hasa katika suala zima la maendeleo. Kuna nyakati hufanya chanya ikazaa hasi na wakati mwingine hasi kuzaa chanya.

Mathalan, inapotaka upanuzi wa barabara au kupitisha barabara au pengine reli mahali fulani, hujikuta imefanya hasi kwa ajili ya kuleta chanya, hubomoa majengo na kusafisha mashamba ya wananchi na kuwaacha wakilia.

Na wanaolia mara nyingi huwa ni waliovamia maeneo lakini kuna wanaochekelea ambao huwa wamefuatwa walikojikita na hivyo kulazimika kulipwa fidia ya mali zilizoharibiwa, na hata kupewa maeneo mengine.

Wapo wanaocheka sana ambao hupewa si tu fidia ya mali zao lakini hujengewa hata nyumba zingine na kuongezwa cha juu. Hao ndio hucheka maisha yao yote.

Si hivyo tu, kuna wale wanaojenga mabondeni na kukumbwa na maafa yatokanayo na mafuriko au maporomoko yasababishwayo na hali ya hewa, hawa ndio wanaohatarisha maisha yao, hivyo serikali kufanya chanya ambao kwao ni hasi.

Serikali huamua kuwavunjia makazi yao na kuwataka watafute kwingine kwa kukaa kwani ni mzigo kuacha watu wako wafe ukiwatazama kwa uzembe wao, ni bora kuwaepushia majanga kwa kuwalazimisha kuhama.

Miaka ya hivi karibuni, tumesikia watu wanahama Ngorongoro kwenda kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga, tukiambiwa watu hawa wanahama kwa hiari na wengine wakionekana kwenye luninga wakikiri kuhama kwa hiari.

Katika hilo, wakaibuka watu kusema serikali inalazimisha watu hao kuhama na hakuna hiari yoyote na eti ni ukiukaji wa haki za binadamu na hata wanaharakati wa haki hizo, wakiibuka na kunyooshea kidole Serikali kuwa si sikivu bali onevu.

Watu waligonganisha vichwa katika suala hili na wengine kugongana kimwili katika eneo la tukio, kila upande ukitaka kuthibitisha ni upi ukweli wa ama hiari au lazima watu kuhama.

Wanasiasa nao wakaingia kila mtu akivutia upande wake wa imani, wenye chama tawala wanaomiliki serikali wakishikilia kuwa ni hiari na wanaotaka kuingia Ikulu, wakisema hakuna lolote bali ni uonevu mtupu, kwani mabavu yanatumika.

Lakini si siri pia kuwa katika mchakato huo kumekuwa na ushawishi fulani ukitolewa kwa sura ya elimu kwa jamii ya Wamasai wanaoishi Ngorongoro, ili waelewe somo la kuhamia Msomera kwa hiari. Imefanikiwa.

Elimu yenyewe ya msingi ni rahisi si tu kuwa watu wamezaliana sana katika Hifadhi hiyo ya Ngorongoro, hivyo kuchanganyana zaidi na wanyamapori na kukaribia kuathiri masuala ya hifadhi na utalii kwa ujumla, hivyo kuwapo haja ya kulitambua na kuliepusha.

Lakini elimu ya sekondari ni hii; na ni kwa mujibu wa 'Mkuu wa Shule', Kamishina wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Ngorongoro (NCAA), Richard Kiiza, kwamba ukikubali kuhama unalipwa stahiki zako za kisheria na motisha juu.

Fidia hiyo ni ya kisheria inayoambatana na ya maendelezo, gharama za usafiri wako na kaya yako pamoja na mali zako zote; kuna malipo ya motisha ambayo si ya kisheria lakini; unapewa nyumba moja kwenye eneo la ukubwa wa ekari mbili na nusu.

Unakabidhiwa shamba la ekari tano, unapigwa na hatimiliki ya kiwanja na shamba lako na unakabidhiwa eneo la malisho ya mifugo yako. Kama haitoshi, unapigwa na kitita cha maokoto ya Sh milioni 10, ukiwa safarini ukielekea makazi mapya, mbonji na msosi unapiga Karatu.

Ukishafika Msonera, unapigwa magunia mawili ya chakula kwa matumizi ya miezi mitatu ya awali ukiwa bado na amba mguuni.

Mungu akupe nini? Hapo ni kama unakwenda Msomnera, lakini kama umehiari kwenda chimbo lingine, unapigwa Sh. milioni 15. Kama si nia nje ya serikali kuboresha maisha yako utaitaje? Milionea wa ghafla au siyo!

Hapo kwa vifurushi hivyo, usihame kwa hiari utakuwa nani basi! Hata mimi ukiniambia nitahama hata sasa, ndiyo sababu nimeghairi ushauri wa Waziri wa Fedha wa kuhamia Bujumbura kukimbia tozo, afadhali niende zangu Msomera.

Nakwambia kwa hiari hiyo, mpaka Jumapili ya Februari 25, mwaka huu, kijijini Msomera kuna vichwa vya watu 6,461 kutoka kaya 1,042 na mifugo 29,919 kama katika siku hizi hawajachinjwa baadhi au kuzaliwa wapya.

Hongereni sana kwa kuhamia Msomera kwa hiari, kwa sababu hiari yashinda utumwa, au siyo! Hiari oyeeee!

## Manispaa yaelemewa na wanafunzi, wakaa chini

**Na Neema Emmanuel,**
ILEMELA

REKODI kubwa ya uandikishaji wanafunzi kuanza masomo kwa mwaka wa masomo wa 2024, imesababisha Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza kuzidiwa, hivyo wengi kukosa madarasa na kukaa chini.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Masala, alithibitisha hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Buswelu katika kikao cha kusikiliza na kutatua kero za wananchi wilayani hapa.

Alisema upungufu huo wa madarasa unasababishwa na idadi kubwa ya wanafunzi kutokana na mwitikio wa wazazi kuwapeleka watoto shuleni, hivyo kufanya idadi kuzidi makisio ya awali.

"Katika kukabiliana na hali hii, tunatarajia kuanza utengenezaji wa madawati awamu ya pili ambayo yatapelekwa katika shule zote ndani ya mwaka huu wa fedha na utekelezaji utaanza Machi, mwaka huu," alisema Masala.

Alisema miongoni mwa shule ambazo wanafunzi wanakaa chini ni Shule ya Msingi Buswelu huku akianza kuongeza shule mpya za Busenga na Bujingwa ambazo zikikamilika watahamishiwa huko.

Aidha, Ofisa Elimu Sekondari wa Manispaa hiyo, Sylvester Mlimi, alitaja mpango wa muda mrefu kuwa ni kuhakikisha wanajenga shule karibu ili kuwapunguzia umbali kwa baadhi ya wanafunzi wanaotoka maeneo yaliyo mbali na shule.

"Maelekezo ya serikali ya sasa hivi ni kuandaa mpango wa kila kijiji au mtaa kuwa na shule, hivyo wananchi tunawaomba tunapohitaji kutumia maeneo yenu kwa suala la elimu, mtoe ushirikiano kwa sababu shule za kata zimezidiwa kwa wingi na umbali umekuwa changamoto huku usafiri kwa wanafunzi ni shida," alisema Mlimi.

Mmoja wa wakazi wa Buswelu, Charles Vedastus, aliiomba serikali kupitia mkuu huyo wa wilaya, kujenga shule ya bweni ili kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu pamoja na kuzuia mimba za utotoni ambazo zinaweza kujitokeza.

# Walimu nguzo muhimu mageuzi elimu

**Na James Mwanamyoto,**

WALIMU ni nguzo muhimu katika kuleta mapinduzi kwenye sekta ya elimu na kwamba serikali inawategemea watumishi wa kada hiyo kutimiza azma hiyo, imeelezwa.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde, alisema hayo huku akitoa wito kwa walimu nchini kote, alipozungumza kwa nyakati tofauti na walimu wa halmashauri za wilaya ya Gairo, Kilosa na Mvomero ambao wanahudhuria mafunzo ya walimu wa masomo ya sayansi na Kiingereza kwa shule za msingi kupitia siku maalumu ya MEWAKA nchini.

"Mwalimu ukiamua unaweza kufanya mambo makubwa sana katika taifa letu na ndiyo maana serikali inawategemea walimu katika kuleta mapinduzi ya elimu ambayo ni moja ya vipaumbele vya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Dk. Msonde alisema azma ya Rais Samia na serikali yake ni kutaka watoto wa kitanzania wapate ujuzi unaostahili na kuongeza kuwa Rais anatarajia wanafunzi wote wa darasa la kwanza, la pili na la tatu, wajue kusoma na kuandika kwa ufasaha.

Alitabanahisha kuwa walimu wakiwafundisha vizuri watoto ni dhahiri kuwa watapata umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu ikiwa ni pamoja na umahiri wa masomo yote wanayofundishwa.

"Mnapofundisha lengo lisiwe kumaliza kurasa za vitabu bali mjikite katika kuhakikisha watoto wanapata ujuzi katika somo husika, hivyo umahiri ndilo jambo la kupewa kipaumbele," alisema.

Dk. Msonde alisema bayana kuwa serikali inawaamini na kuwathamini walimu wote nchini ndiyo maana inajali maslahi yao, hivyo ni jukumu lao kuamua kutekeleza wajibu wao kikamilifu kwa mustakabali wa elimu na maslahi ya taifa.

Jumla ya walimu 60,036 nchini wanahudhuria mafunzo ya walimu wa masomo ya sayansi na Kiingereza kwa shule za msingi kupitia siku maalumu ya MEWAKA kupitia vituo mbalimbali vilivyoko katika wilaya zao.




Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde akizungumza na walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa jana, wanaohudhuria mafunzo ya walimu wa masomo ya sayansi na kiingereza kwa shule za msingi kupitia siku maalumu ya MEWAKA nchini. **PICHA: JAMES MWANAMYOTO.**

## Mwanafunzi alazwa kwa kung'atwa nyoka akilima shamba la mwalimu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Minandi, Ikungi mkoani Singida, Felista Charles (16), amelazwa katika Hospitali Teule ya Makiungu kwa zaidi ya mwezi sasa baada ya kung'atwa na nyoka wakati akilima katika shamba la mwalimu mmoja wa shule hiyo.

Akizungumza katika mahojiano na gazeti hili juzi katika wodi namba 14 kwenye hospitali hiyo, mama mzazi wa mwanafunzi huyo, Cecilia Neriko, alisema mtoto wake aling'atwa na nyoka Januari 23, mwaka huu, katika mguu wa kulia wakati akilima kwenye shamba la mwalimu wa shule hiyo aliyefahamika kwa jina la Robert.

Alisema baada ya tukio hilo, walimu wa shule hiyo walimpeleka kwa mganga wa kienyeji, maarufu kama Njoka, ambaye anaaminika anatibu wagonjwa waliong'atwa na nyoka lakini alishindwa kumtibu kwa kuwa sumu ya nyoka ilikuwa imeanza kusambaa na mguu kuvimba. Neriko alisema baada ya hali ya mwanafunzi kuwa mbaya, ndipo wazazi walijulishwa na baba mzazi, Charles James, alikwenda kwa mganga huyo wa kienyeji kumchukua kwa pikipiki lakini kutokana na hali ya mtoto kuzidi kuwa mbaya na kushindwa kukaa kwenye pikipiki, walilazimika kukodi gari na kumpeleka katika hospitali ya Makiungu.

Alisema mwanafunzi huyo alipelekwa katika hospitali hiyo Januari 24, mwaka huu, na siku iliyofuata (Januari 25) alifanyiwa operesheni ya mguu kuondoa baadhi ya nyama kwenye mguu ili kuzuia sumu ya nyoka kuendelea kusambaa mwilini.

"Hali yake si mbaya sana japo bado hawezi kutembea. Ameshonwa nyuzi kadhaa imebaki sehemu nyingine hajashonwa wanasubiri ikauke na madaktari wameshauri awe anakula mayai, maziwa machachu na samaki," alisema.

Mzazi huyo alisema licha ya tukio hilo kumpata mwanawe wakati akilima shamba la mwalimu, mkuu wa shule hiyo hajawahi kufika hospitalini kumjulia hali na gharama za matibabu yake zinabebwa na wazazi tangu alipolazwa.

Alisema Mwalimu Robert ambaye mwanafunzi alipata tukio hilo wakati akilima shamba lake, ndiye huwa anakwenda kumjulia hali na Januari 28, 2024 alipofika hospitalini, alitoa Sh. 54,000 kusaidia matumizi ya mgonjwa.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Miandi, Juma Maati, alipotafutwa kwa siku tatu kupitia simu yake ya mkononi, alikuwa hapatikani na Mwalimu Robert kila alipotafutwa, simu yake ilikuwa ikiita na kukata na baadaye alituma ujumbe mfupi wa maneno (sms) kwamba ana taarifa za mwanafunzi huyo kung'atwa na nyoka.


Baba huyo wa mwanafunzi, alisema hali ya mtoto wake ilikuwa mbaya na kuna kipindi alilazwa katika chumba maalum cha uangalizi (ICU) na kwamba kama wangechelewa kumwahisha hospitalini, mambo yangekuwa mengine.

# MAISHA

MACHI 3, 2024
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




## SINGLET VAZI LISILOPOA

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | 5 | 8 | 7 | 5 | 8 | 5 | A | 4 | 9 | 0 | |
| 9 | 6 | 9 | 6 | 7 | 9 | 4 | 3 | 8 | 0 | 8 | |
| 5 | 8 | 5 | 8 | 5 | 8 | 7 | C | 9 | 0 | 2 | |
| 1 | I | 9 | 8 | 9 | 4 | 8 | 9 | 4 | 4 | 8 | 9 |
| 5 | 9 | 6 | 8 | 2 | 8 | 1 | 3 | 8 | 5 | 8 | |
| 3 | 8 | 9 | 4 | 8 | H | 8 | 8 | 0 | 3 | 3 | |
| 8 | 5 | 9 | 4 | 8 | 0 | 8 | 0 | 3 | 8 | 2 | |

CHAI

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | P | U | N | J | E |
| B | | | | Y | | N |
| W | | B | A | O | | D |
| A | N | A | | T | E | E |
| B | | N | O | A | | L |
| W | | D | | | | E |
| A | M | A | N | I | | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

NOA, BAA, BEI, AGA, UKOKO, JESHI, SHABA, BANGO, MSTAAFU, INJINIA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

WATOTO wawili Juma na James walikuwa wakienda porini kutafuta vipepeo.

Walipokuwa porini Juma na James walianza kufundishana namna ya kuwakamata vipepeo bila ya kuwadhuru.

Juma: Niliambiwa na mama kuwa vipepeo ni viumbe vizuri

James: Hata mama yangu aliniambia lakini alisema ni dhaifu wakati wa kuwakamata.

Juma: Kama ni dhaifu kwa nini tumekuja kuwakamata? Ni bora kuwaacha tu kwani tutaonekana sisi sio majasiri.

James: Sina maana hiyo, yaani mbawa zake zinatoka kwa urahisi.

**SWALI**

Kilimo cha miti ya mbao kinapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mke alienda kusalimia, ndugu wakamnyima kurudi kwangu!

PENZI msomaji, hebu tuendelee kusikia vilio vya wenzetu ndani ya ndoa zao. Usione watu wanatabasamu barabarani na kuvalia nadhifu, kumbe moyoni wana maumivu makali ila tu wafanyeje. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Hebu wasikie hawa wasomaji wetu kama walivyonitumia vilio vyao kupitia ujumbe mfupi kwenye Email yangu fwingia@gmail.com, kisha tujadiliane.

Mmoja anasema hivi; Naitwa Aloisi Adolfu umri wangu miaka 47 naishi Moshi Vijijini. Nina tatizo la kukimbiwa na mke wangu wa ndoa tuliyofunga mwaka 2003 Singida tulikokuwa tunaishi kwa miaka 10 ambapo tulijaliwa kupata watoto wawili wa kiume.

Nilikuwa mfanyabiashara na nilipoishiwa akanikimbia mwaka 2012 sasa ni miaka miwili nimesikia yupo Arusha na bwana mwingine. Wazazi wake ni majirani zangu.

Nifanyeje? Nimeshajenga nyumba natarajia kufungua duka. Mtoto mmoja yuko naye na yule mkubwa nipo naye. Naomba ushauri mke huyo hajatulia".

Msomaji mwingine anasema hivi kwenye ujumbe wake wa simu; Kwa mfano mwanamke ameamua kwenda kwao kwa matatizo madogo ya kindoa pamoja na watoto.

Baadae mume anagundua kaenda kwao kisha anamfuata. Ndugu zake wanamkatazia asirudi kwa mume. Eti kwamba huwezi kumchukua ila tambua kuwa huyu ni mkeo na hawa ni watoto wako.

Baada ya kujibiwa hivyo mume anaondoka zake. Je, asipotunza ile familia atapata laana? (Msomaji kutoka Njombe, Iringa).

Mpenzi msomaji, bila shaka umewasikia wenzetu hao, mmoja ndoa imeparaganyika mke kule, mume huku na kila mmoja akajikuta anabakia na mtoto mmoja, mwingine anatoa fumbo lakini ni mfano halisi uliotokea yawezekana ni kwake au kwa jamaa yake.

Naam. Tukianzia ya jamaa aliyekimbiwa na mke utagundua kuwa kuporomoka kwa uchumi kwa mume yule ndiko kulikosababisha mke kumkimbia. Lakini mke yule alisahau kwamba katika biashara kuna kupata na kukosa kutegemeana na mazingira ya biashara yenyewe. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Kwa mantiki hiyo, mke huyu alipaswa kuwa mzalendo kwa mumewe na kuwa mvumilivu na zaidi kumfariji mume katika wakati huo mgumu wa anguko la biashara zake na siyo kumbikimbia. Ukiona hivyo, mke huyu alidhamiria na pengine alikuwa na ile roho ya kumchoka mwenzake, hivyo kutaka kuangaza kwingine, jambo ambalo lilifanya. Tayari mumewe ana fununu kuwa anaye mwanaume mwingine huko Arusha.

Inavyoonekana, mama huyo anaona kuwa tayari wameshagawana watoto hivyo hana muda tena na mumewe na ndiyo maana ametafuta mwingine, tena mbali. Hata hivyo hatua aliyochukua siyo sahihi.

Binafsi nauita usaliti wa hali ya juu. Mbona hakukimbia wakati mumewe akiwa na afya njema kiuchumi? Je, alikuwa akimpenda mumewe kwa kuwa alikuwa na fedha tu?

Je, ile ahadi ya kupendana kwa taabu na raha aliyoiweka madhabahuni wakati wa kufunga ndoa mbona ameivunja? Hawa ndio wale wanaokupenda pale tu unapokuwa na kitu, ukifilisika wanakukimbia.

Huo mfano mwingine mke kwenda kwao nduguze wakamkatalia asirudi ila eti atambue kuwa wale watoto ni wa kwake, nao una mushkeli.

Ukiona vile ni dhahiri ilikuwepo mipango kabla ya mwanamke huyo kuondoka na pindi atakaponyanyua mguu asirudi tena.

Sababu za kubomoka ndoa ni nyingi. Moja ni eneo la uchumi kwa mfano wa kwanza hapo juu. Ndugu nao wamechangia sana katika kutikisha ndoa. Wakwe na mawifi ni shida nyingine kwa kuingilia ndoa nyingi.

Mwanamke au mwanaume anapaswa kusimama na kuiombea familia yake. Hivi sasa shetani ameshikilia maeneo makubwa manne ambayo anayatumia sana kubomoa familia nyingi. 1. Ndoa 2. Uchumi 3. Afya na 4. Watoto.

Sehemu hizo nne ndizo anazotumia zaidi kuhakikisha kuwa hakuna amani na utulivu ndani ya familia zetu. Sote tukishalijua hilo, yatupasa kusimama na kutafuta uso wa Mungu ili kutufungua na hatimaye kujua chimbuko la yote.

Haiwezekani kwa mfano, mke au mume uliyemchagua kwa moyo mmoja mkasimama madhabahuni lakini baada ya muda mfupi kila mmoja anamuona mwenzake kama takataka. Haiwezekani!

Hizo ni hila za shetani, lakini tukisimama tukimwita Mungu aingilie kati hakuna linaloshindikana kwa sababu tayari ameshatuambia katika neno lake kwamba tukimuomba neno lolote kwa jina lake atatupatia.

**Je, una maoni kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Mbokomu mna shida gani lakini?

UKIENDA katika Mahakama za Mwanzo katika ukanda wa juu wa Old Moshi, mkoani Kilimanjaro, nusu ya wahalifu wanaopandishwa kizimbani wanatoka Mbokomu.

Ukienda Mbokomu, mahame ni mengi (magofu ya nyumba).

Ni kwa nini wanahama? Jibu ni rahisi tu kwamba hakuna huduma muhimu za kijamii.

Hakuna hoteli, daladala zinazoanzia katikati ya mji, yaani kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini, migahawa, wala nyumba za kulala wageni hakuna.

Hiyo ni Mbokomu ambayo imetoa vigogo serikalini wenye mchango mkubwa kwa taifa letu. Wako wale wanaoitwa 'business tycoons' wametelekeza kwao.

Wafanyabiashara wakubwa wenye majina, wadau wa sekta ya michezo nchini, wenye majina na utajiri wa kufuru, wamejaa Dar es Salaam na majiji yetu mengine matano, wameipa mgongo Mbokomu.

Lakini hadi leo, zaidi ya miaka 60 ya Uhuru, Mbokomu haina kituo cha afya, haina barabara ya lami au ya kiwango cha changarawe inayopitika kwa uhakika.

Leo hii ndio wamepata Kituo Kidogo cha Polisi, tena baada ya wazawa kujichangisha huko mikoani.

Ukienda Mbokomu, hizo nyumba utakazoziona barabarani, miaka ya nyuma yalikuwa maduka, kulikuwa na soko, kulikuwa na mabasi ya SHIMATSO, sasa hivi hakuna. Vijana wakimaliza shule wakiondoka harudi.

Akijitokeza mzawa kutafuta mwarobaini wa maendeleo ya Mbokomu mnamwita mpinzani, mwanaharakati. Mna nini lakini?

Labda shida ya Mbokomu ilianzia hapa. Nawaza tu kwa sauti!

Wenyeji wanakuambia kila uchao, lori lililobeba pombe aina ya bia, lenye mzigo wa kati ya Sh. milioni saba na 10, linapita Mbokomu na bia zinaisha kila siku.

Lakini nyama ya ng'ombe, ukichinja katika vijiji vinne vya Kata ya Mbokomu, ambavyo ni Korini Juu, Korini Kati, Korini Kusini na Tema, anzia pale lilipo soko la zamani la mitumba la Kiborloni.

Acha mguu wa nyuma wa nyama ya ng'ombe, nenda Saoni acha kichwa, Fukeni acha mguu wa nyuma, Tema acha mguu wa mbele, Kiwalaa, acha mguu wa mbele, hiyo nyama haitanunulliwa yote. Kifupi haitaisha.

Mbokomu ni Kata ya mwisho kwa maendeleo katika Jimbo la Moshi Vijijini, kwa sababu ya unafiki uliopo.

Wenyeji wenyewe kwa wenyewe, wanaambiana mnafiki anazaa mtoto mnafiki na mjukuu mnafiki.

Wana Mbokomu, hebu tubadilike. Tujipende na tuache mauzauza, tukumbuke kuwekeza kwetu. Nyumbani kwanza.

Halafu mambo ya kuitana wapinzani yanatoka wapi? Ndiyo maana mnapitwa na kata jirani, kwa sababu ya haya mambo haya! Ni aibu. Leo ukienda Mbokomu na shilingi milioni moja, unaweza kulala na njaa.

Labda urudi Kiborloni. Hakuna mahali pa kufanya matumizi, bar ya ukweli, mgahawa wa kisasa, lodge na kumbi za harusi au mikutano.

Mbokomu kuna ulevi wa kupitiliza, ulevi wa kupindukia. Tengenezeni sheria ndogo za kudhibiti muda wa kunywa pombe. Gongo, pombe za vibobo huko ndiko nyumbani kwake, zimelala.

Wanaoijua Mbokomu ya sasa, wanasema afadhali ya yale mambo yaliyokuwa yakizungumzwa kipindi kile kuwaathiri wanaume wa wilaya ya Rombo.

Haiingii akilini, asubuhi kijana anaonekana amelewa, kijana mdogo anaonekana ana umri mkubwa. Amezeeka kuliko hata wazee. Kumbe ni matumizi ya hovyo ya gongo na pombe za vibobo.

Kuna wazee na kinamama wazawa, ambao ni waasisi wa New Mbokomu Development Group, mnawabeza lakini wanaweza kuwa 'taa' kwenu.

Nyie nyie wazawa wa Mbokomu, rudisheni nguvu nyumbani, acheni kupigana vita isiyopiganiwa na Mungu. Changamkieni fursa za uwekezaji kwenye Kata yenu.

Utalii utawabeba nyumbani kwenu mmepakana na Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA). Mnao mti mrefu kuliko yote Afrika, uko nafasi ya tatu duniani, mnafeli wapi?

Jengeni basi hoteli na nyumba za kisasa za kulaza wageni, hapa ni karibu sana na mji wa Moshi.

Kili Marathon ni mashindano yenye hadhi ya kimataifa, yanavuta mamia kwa maelfu ya watu, wakiwamo raia wa kigeni kuja kukimbia kila Februari.

Kili Marathon ya majuzi, iliweka rekodi kwa mara kwanza ya kuingiza zaidi ya watu 11,000 katika Mji wa Moshi.

Wageni walifurika wakakosa nafasi za kulala, wakakimbilia miji ya jirani, hasa wilaya ya Hai. Nyie mnayo ardhi ambayo haijaendelezwa zaidi ya migomba na kahawa.


Mngekuwa na lodge za kisasa, pesa zingependezesha mji wenu, vijana wangepata ajira, wazee wangeongeza umri wa kuishi aisee!

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI









Februari 23, ilikuwa siku ya furaha na muhimu katika maisha ya Faraji Mgeni 'Kipunje' na mkewe, Pendo Juma Kassim baada ya kufunga ndoa na kufuatiwa na sherehe ya kuwapongeza iliyofanyika nyumbani kwao Tegeta Bwawani mkoani Dar es Salaam.

# MITINDO



# SINGLET VAZI LISILOPOA



VAZI la 'Singlet' ya mazoezi limekuwa maarufu kwa wanaume hasa kwa ajili ya kuonyesha maumbo yao kikamilifu.

Awali ilifahamika Singlet ni moja ya vazi la ndani kabla ya kuvaa vazi rasmi, lakini kwa sasa aina hiyo ya nguo imeboreshwa na kutumika sehemu za wazi hasa kwenye mazoezi.

Hakuna ubishi kwamba wanaume wanapovaa vazi hili huonekana wenye nguvu, anayejiamini na aliyekamilika kiasili.

Hata hivyo, kutokana na kuonyesha sehemu kubwa ya mabegani na kifua kuwa wazi, ni muhimu kwa mvaaji kuwa msafi.

Usafi wa nguo na mwili ni mambo yanayozingatiwa kila unapohitaji kuvaa Singlet pale unapotaka kwenda katika mazoezi au matembezi ya jioni.

Pia ni vizuri kuhakikisha usafi wa kwapa ili kuweka singlet katika hali ya usafi muda wote na isiwe tabu kwako kuinua mkono kwani wengi wanakuwa hawana uhuru kwa kuficha kwapa zao kutokana na uchafu.

Nguo hizi unatakiwa kuwa na machaguo mazuri kutokana na rangi, ubora na mtindo wake.

URAMBO

UREMBO

Na Mary Geofrey

# USO MARIDADI

## Tumia dawa ya meno ujionee

CHUNUSI hutokea pale seli za ngozi zilizokufa au mafuta yanapoziba vioteo vya nywele.

Pale mafuta yanayoendelea kukusanyika husababisha kuvimba na kusababisha maumivu kwa eneo la mwili lililoathirika.

Tatizo la chunusi mara nyingi huanza katika ujana, kutokana na homoni zinazoanza kuzunguka mwilini wakati wa kubalehe. Mara nyingi chunusi hupungua katika utu uzima ingawa wakati mwingine zinaweza kudumu kwa muda mrefu.

Wakati mwingine chunusi zinaweza kurithiwa.

Hata hivyo, matumizi ya krimu au mafuta mazito yanayoziba vinyweleo wakati mwingine huchochea chunusi kutokea.

Watu wenye matatizo ya homoni wana uwezekano mkubwa zaidi wa kupata chunusi.


Kuondoa mabaka mabaka ya chunusi au makovu ya magonjwa ya ngozi, inaweza kuwashangaza wengi, lakini nawashauri jaribu.

Ili kuondoa tatizo hilo ni vyema mtu mwenye tatizo hilo akatumia dawa ya meno yoyote wakati usiku.

Kinachotakiwa kufanya ni kupaka dawa ya meno kwenye maeneo yaliyoathirika na mabaka mabaka ya chunusi au maradhi ya ngozi kabla ya kulala halafu asubuhi unasafisha uso wako vizuri na sabuni.

Kisha acha uso wako ukauke vizuri na upake mafuta uliyozoea kupaka.

Rudia kupaka dawa ya meno kwa siku tano na utaona madoa yote yamepotea usoni na utabaki na ngozi yako isiyo na makovu.





MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Juisi ya ukwaju

UKITAKA kuingiza vitamin B, C, K mwilini unatakiwa kufanya jambo moja tu, nalo ni kutengeneza juisi ya ukwaju.

Juisi ya ukwaju haina gharama ukilinganisha na aina nyingine, ina mahitaji machache na inafaa sana kwa watu wenye familia kubwa.

Fuatana nami ujifunze na kuongeza ujuzi wa kutengeneza juisi ya ukwaju.

**Mahitaji**

Ukwaju nusu kikombe, sukari robo kikombe, iriki, vanilla robo kijiko

**Maandalizi**

Hatua ya kwanza kwenye uandaaji wa juisi hii ukishanunua ni kuuloweka ukwaju kwenye maji kiasi.

Baada ya dakika 10 anza kuukoroga kwa kutumia mwiko au kijiko kisha bandika jikoni mpaka uchemke.

Ongeza sukari nusu kikombe au zaidi kutegemea na wingi wa juisi yako

Weka vanila robo kijiko, pamoja na hiriki kama utapendelea.

Baada ya dakika tano sukari ikichanganyika vizuri epua na uchuje kisha acha ipoe.

Baada ya kupoa unaweza kuweka kwenye friji ipate ubaridi kidogo au unaweza kuongeza vipande vya barafu na juisi yako itakuwa tayari kwa kunywa.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Dondoo za faida uwekezaji wa nyumba



UJENZI wa nyumba ni miongoni mwa mambo muhimu yanayotumiwa na watu wengi kuwekeza.

Uwekezaji ni mchakato mzima wa kuiweka mali katika mfumo maalum wa kifedha kwa ajili ya tija zaidi ya baadaye ambayo inaweza kuongezeka au namna fulani yenye kuleta faida baada ya muda maalumu uliyowekwa.

Leonald Michal, mshauri wa masuala ya uwekezaji, anaelezea kanuni bora za kuwekeza kwa tija kwenye nyumba.

Anashauri kwamba unapowekeza kwenye ujenzi wa nyumba miongoni mwa mambo ya kuzingatia ni pamoja na kujua unataka kujenga nini kulingana na mahitaji katika uhalisia wa sasa na wa baadaye.

"Kutazama ni aina gani ya watu watakaotumia nyumba yako, shughuli gani ambazo zitakuwa zinafanyika katika nyumba husika.Kwa hiyo ni muhimu pia kushirikiana na mtaalamu aliyebobea katika usanifu.

"Pia kujenga kwa kuzidi uwezo wako huleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi, sehemu nyingine kutotumika na kutokuwa na faida ya kutosha, kutumia pesa nyingi kwa kitu kisicho na faida na kuwa na gharama kubwa za uendeshaji wa jengo."

"Kujenga kwa kutokidhi mahitaji, huleta hasara kwa kulazimika kufanya upanuzi wenye gharama kubwa zaidi, kuacha nyumba na kutafuta nyingine, kutoridhika na kutokuwa huru zaidi.Ni muhimu kuhakikisha kwamba unachojenga kitaleta faida kwa kipindi hicho cha uwekezaji," anasema.



Anashauri kwamba ni vyema kujiuliza maswali kama je, kodi ambayo wapangaji wanailipa inaleta faida? Mtaji uliotumia kujengea utakuja kujilipa baada ya muda gani? Faida ya kifedha itaanza kupatikana baada ya muda gani? Na je, nyumba yako itadumu kwa miaka mingapi?

Jambo lingine muhimu, anasema unapowekeza katika nyumba ni kufuata sheria na taratibu zote husika ili uwekezaji wako usibughudhiwe na mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuhatarisha mchakato wa kupata faida kwa kujenga katika eneo linaloruhusiwa kisheria na kwa kufuata sheria na taratibu zote.

Pia anasema makadirio ya gharama za ujenzi yatakusaidia namna ya kujipanga juu ya mtaji wa kukuwezesha kusogeza mbele na kazi yako na kwamba si vyema kujenga kwa kubahatisha.

"Ni muhimu kuiona faida katika mipango yako ambayo umeifanya kabla ya kuanza ujenzi," anasisitiza.

## DONDOO

# Tairi za zamani hazitupwi

**Na Restuta James**

KAMA unahitaji mawazo mapya ya kutengeneza mandhari ya nyumba yako, yenye ubunifu kwa gharama nafuu, usiache kuangalia tairi ya zamani.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa tairi za zamani ni zana muhimu ya kukuwezesha kuwa na bustani maridadi kwa gharama ndogo.

Mtaalamu Lameck Petro, anasema tairi hizo zinafaa kutumika kama nakshi ya sinki la kunawia mikono, kiti, stuli na chombo cha kupandia maua. Pia yanafaa kwa kuweka mpaka na kunogesha mpangilio kwenye eneo la wazi.

"Ni pambo zuri la kufurahisha kuanzia kiti hadi sinki la kunawia. Unaweza kupaka rangi uzipendazo kulingana na matumizi yako," anasema.

Anasema tairi zinaweza kupangwa mstari na kugawa eneo la bustani kisha zikapakwa rangi aipendayo mwenye nyumba au katika eneo la mgahawa.


Anapendekeza kuwa rangi nyeupe inafaa zaidi kupakwa kwenye tairi za kugawa eneo wakati zile za kupandia maua zinaweza kupakwa rangi mchanganyiko au moja kadiri mtu apendavyo.

Hata hivyo, Lameck anasema kwa matumizi ya sehemu ya kunawia mikono, tairi linaweza kuachwa na rangi yake ya awali. Kadhalika, anasema kama mwenye nyumba anaweka tairi zaidi ya tano, anaweza kuzipaka rangi baadhi na nyingine zikabakia nyeusi.

"Kwa wanaotaka kutumia kama kiti au stuli, unaweza kuweka ubao juu yake na kuweka miguu na pia unaweza kuzijengea kwenye eneo lako la kupumzika. Tairi za zamani siku hizi hazitupwi," anasema.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
KASHESHE
ACHA HILA HAPA UPO UKWENI HUONI AIBU?
AIBU WANGEONA 'KUNGUNI' WANAONICHANGAMKIA KAMA KEKI YA BESDEI.
...HADUBINI...
EBU'ACHA WAZIMU UNAJUA KUWA 'DEMU' TUNAYEMGOMBANIA KACHINJWA LEO NA SISI KESHO?
USINIPIGE'SIASA ALIYECHINJWA SIO YEYE BHANA!
NDANI YA KIBASI
HIVI DEREVA UNAVYOKIMBIZA GARI HUONI KAMA NI HATARI?
EBU' MWACHE DEREVA ATIMIZE WAJIBU WAKE AKIMBIZE GARI KWANI LIMEMUACHA?
MCHAWI YUPO MBELE
WEWE UNAYETETEA NDIO MNAKUWAGA WA KWANZA KUKATIKA KICHWA KIKAPOTEA!
USINIHANGAISHE! TUNAZUNGUKA KOTE MBONA HATUFIKI ULIKOLALA?
NILIENDA USIKU ALAFU NIMELEWA CHAKALI PIA UMEME ULIKATIKA GIZA TOTORO ILA TUSICHOKE!
KIWESE KIMEKATA NA MFUKO NAO UMEKATA 'KWELI BIA SHIKAMOO' UMEJUA KUNIKAMUA!
VIONGOZI WETU WA DINI WALIPOSEMA TULINDE NDOA ZETU KWA GHARAMA YOYOTE ULIELEWAJE?
UNATAKA NIJIBU VIBAYA UNITAWANYE UBONGO!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
HATA UKILIA ULIYEMUACHA KABEBWA...

MAZISHI YA MZEE RUKHSA

# MATUKIO YA KUAGWA KWA MWILI WA RAIS MSTAAFU HAYATI ALI HASSAN MWINYI MJINI ZANZIBAR



Viongozi wastaafu mbalimbali wakiwemo Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na Marais wastaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Amani Abeid Karume, wakiwa katika hafla ya kuuaga mwili wa Rais mstaafu wa Hayati Ali Hassan Mwinyi katika Uwanja wa Amani, mjini Zanzibar jana, kabla ya maziko yake yaliyofanyika katika kijiji cha Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA ZOTE: IKULU**



Maofisa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakiwa wamebeba jeneza lenye Mwili wa Rais mstaafu Hayati Ali Hassan Mwinyi, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Amani jana.



Rais Samia Suluhu Hassan, akijadiliana jambo na Makamu wa Rais wa Namibia, Netumbo Nandi Ndaitwah (wa pili kushoto). Wengine ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.



Sehemu ya wananchi waliohudhuria hafla hiyo.



Sehemu ya wanafamilia wakiwepo wajane wa Hayati Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, Mama Siti Mwinyi (kushoto) na Mama Khadija Mwinyi (wa pili kushoto), Mama Maryam Mwinyi ambaye ni Mke wa Rais wa Zanzibar na Mtoto wa marehemu, Abdullah Mwinyi, wakiwa katika hafla hiyo

## MAKALA

# UTAJIRI NA UMASKINI KIKWAZO CHA MAENDELEO



Na Magabilo Masambu

**Kwa kauli hiyo, anataka tumpe nafasi atusaidie kwa sababu shida anazijua. Ni kweli inawezekana shida unazijua, hilo ni jambo moja, lakini kutotumia nafasi yako ya madaraka kuondoa umaskini wako ni jambo lingine japo si wote wanafanya hivyo.**

ZAMANI palikuwa na mtu mmoja aliyesifika sana katika kuoka mikate. Kilichowashangaza wateja wake na watu wengine katika kijiji kile ni kwamba mwoka mikate huyu kadri alivyokuwa akifanya kazi yake, ndivyo alivyoonekana kukonda zaidi. Baadhi ya watu walipofanya utafiti kwa nini alionekana hivyo, wakagundua kwamba sababu ni njaa.

Swali kubwa likajitokeza, inawezekanaje mwoka mikate akonde kwa njaa ikiwa yeye ndiye mpika mikate? Ina maana anawauzia wengine mikate lakini yeye hali? Je, anakosa muda wa kula au anathamini fedha zaidi anazozipata kwa kuuza mikate au anawajali sana wateja wake?

Ni kweli kwamba iwapo mwoka mikate ataamua kula mikate anayozalisha, uwezekano mkubwa wa wateja wake kuikosa ni mkubwa. Kwanza, wanaweza kukosa kwa sababu anaweza kuvimbiwa akashindwa kuoka.

Pili, anaweza kuoka kweli lakini akala akamaliza. Lakini vilevile ni busara zaidi kwa mwoka mikate kuwa ameshiba kwanza, ili awe na nguvu zaidi ya kuoka mikate mingi.

Katika nchi yetu, kwa miongo kadhaa tumekuwa na dhana ya kuamini kwamba viongozi wazuri ni wale wanaotoka katika familia masikini, ndiyo maana kila kiongozi anapotaka nafasi za kuchaguliwa, husikika akisema kwamba yeye ni mtoto wa maskini na kwamba maisha yetu ameyaishi.

Kwa kauli hiyo, anataka tumpe nafasi atusaidie kwa sababu shida anazijua.

Ni kweli inawezekana shida unazijua, hilo ni jambo moja, lakini kutotumia nafasi yako ya madaraka kuondoa umaskini wako ni jambo lingine japo si wote wanafanya hivyo.

Upande wa pili, tumekuwa na hofu na walioshiba, yaani wenye mali na kwamba tukiwapa nafasi watatumia nafasi hiyo kujilimbikizia zaidi.

Maana yake ukiwa huna mali ni tabu, ukiwa na mali shida. Kosa kubwa tunalofanya ni kuwapima watu kwa umasikini au utajiri wa mali, lakini masuala ya uongozi watu wanapaswa kuwa wameshiba zaidi katika eneo la fikra, utambuzi (maarifa) na uzalendo.

Ziko wapi leo shule za uongozi? Au kinachotuongoza zaidi ni visomo vikubwa pekee visivyohusiana na uongozi? Yako wapi leo maadili na miiko ya uongozi? Maneno matakatifu yanasema: "Mtu hawezi kuishi kwa mkate tu, bali neno la uzima." Neno la uzima katika uongozi ni maarifa lakini maarifa yenyewe yasiwe ya kutuibia.

Kwa hiyo kabla ya kuoka mikate, yafaa tuwe tumeshiba kwanza ili tupate nafasi bora ya kuwahudimia wateja wetu na kuepusha kutumia nafasi hizo kula mikate ya wateja na mwisho wa siku wateja watakufa kwa njaa au sisi tutakufa kwa njaa kwa sababu tutakosa mapato yatokanayo na uuzaji wa mikate, maana sasa wa kuwauzia hawapo.

Kinachoonekana kwa kipindi kirefu na sasa ni kwamba nafasi za uongozi ni mahali pekee pa kupata utajiri.

Itatuchukua miaka mingi sana kuinua hali za watu wetu. Yako malalamiko huko mtaani.

Unakuta kuna mfadhili mahali fulani anataka kusaidia jambo fulani ama kutengeneza barabara au kuchimba kisima.

Viongozi wenye njaa ndio wanakuwa wa kwanza kukwamisha mradi na ninaposema wenye njaa ni wote, wenye mali na maskini wote nia yao kubwa inaonekana ni kutumia nafasi ya madaraka ama kupata au kujiongezea bila kujali shida za wananchi wengine.

Wanakwamishaje? Eti mpaka mfadhili awape kwanza 'teni pasenti' waweke mifukoni ndipo jambo lifanyike.

Tunawanyima maendeleo wananchi kwa sababu ya njaa zetu. Hiyo ni aibu sana kwamba mtu mmoja anaweza kuzuia maendeleo ya kijiji kizima, halafu ukifika wakati wa uchaguzi anakuja tena anasema mimi ni mtoto wa maskini, nichagueni nazijua shida kumbe shida ni yeye mwenyewe.

Nafikiri sasa kwenye kampeni muwe mnatumbia tu ukweli kwamba nichagueni maana watoto wangu wameshindwa kwenda shuleni, sjafanya hiki na kile ili tunapokuwa tunawapa nafasi basi tusiwadai baadaye maana tayari tunafahamu kwamba fedha zetu za maendeleo zinamatumizi mengine.

Nayazungumza haya kwa sababu mwaka huu ni wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Ni uchaguzi muhimu zaidi kuliko uchaguzi mkuu, kwa sababu moja, unatafsiri uchaguzi mkuu na pili, viongozi wa serikali za mitaa ndio tunaokuwa nao karibu katika maeneo yetu.

Baadhi ya viongozi sasa wameanza kupitapita huko kwenye vijiwe vya kahawa, huku wakijifanya maisha yao ndiyo yetu.

Wachunguzeni vyema kwani kila vinapokaribia vipindi vya uchaguzi, maigizo na dhihaka nyingi zinafanyika wakilenga kushinda uchaguzi na baada tu ya kuchaguliwa, wanapotea na kujitokeza sasa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Watoto wamekimbia umebaki na wajukuu, pia watasambaa*



Na Adam Fungamwango

**Miaka ikazidi kusonga mbele, mara tabia ya mwanamke ikaanza kubadika. Akaanza kuwa na kidomodomo, kususa, maneno mengi, kashfa, dharau, kejeli, ili mradi tu nyumba tena haikuwa na amani.**

WAKATI mwingine ndani ya familia kunakuwa na vitu vya ajabu sana. Unakuta hata ndugu wa baba na mama mmoja wanagombana mpaka wanaapizana wasizikane.

Hii inatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo tofauti ya vipato baina yao na dharau kwa wale wenye nacho. Mazingira pia yanasababisha kugombana hasa kila mmoja anapokuwa na familia yake.

Mke na mume wanaweza pia kumbadilisha ndugu tabia, akaanza 'bifu' na ndugu zake bila sababu yoyote. Inawezekana pia hata wazazi wanaweza kuchangia watoto wa baba na mama mmoja kuchukiana.

Kuna baadhi ya wazazi wana ubaguzi sana. Wanawathamini sana watoto wenye kipato na kuwadharau wale ambao hawana kitu. Tabia hii husababisha manung'uniko na mpasuko mkubwa kwenye familia.

Sasa kuna tabia za wale wazazi watu wazima ovyo. Hawa ni baadhi ya wazazi ambao wanafanya vitu vya kusambaratisha wenyewe familia zao. Wako wazazi ambao wanashindwa malezi kwa watoto wao kiasi kwamba wanapofika umri ambao wanaweza tu kujitegemea wanaondoka na kwenda kutafuta maisha sehemu nyingine.

Inavyotakiwa ni kwamba mtoto akitoka nyumbani iwe tayari ameshatengenezewa msingi na kwenda kujitegemea na si kuondoka tu kwa sababu kuna matatizo ya nyumbani.

Wazazi wengine wanawafukuza watoto zao nyumbani kwa sababu tu ya kukwepa majukumu ya kuwalea.

Haya mambo yapo sana kwenye jamii yetu ya Kitanzania na Afrika kwa ujumla, ndiyo maana hata mwanamuziki raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, aliyekuwa akipiga muziki nchini Tanzania, alitunga wimbo aliouita 'Mpakamanga Mbaya.'

Ina maana ameliona hili iwe Tanzania na DRC, na kulitengenezea wimbo ili iwe fundisho kwa wazazi wengine. Hebu soka mashairi ya wimbo huo.

"Oooh Mpakamanga, watoto umemaliza, utakula na nani? Sasa uko pekee. Ubaya wako unajulikana oooh papa. Ubaya wako sasa umemaliza familia. Fikiria mbele, siku zinazokuja, utaishi nani, oooh Mpakamanga, utateseka wakati utakuwa mzee, familia yako sasa wameshaanza kukutambua. Usemi wako utakuwa hauna msaada.

"Watoto umefukuza, mama yao katoroka, sasa usingizi, hauupati, kulala kwa vidonge, ndoto hauoni, mchana huna raha kwa sababu unaishi pekee, ooh Mpakamanga, hongera Mpakamanga, kazi yako nzuri, sasa umekwisha."

Mpakamanga amewatimua watoto wake nyumbani, kiasi cha kumkera mkewe naye akatoroka. Sasa amekuwa mpweke, rafiki zake wanamuuliza, akishafikia uzee ambao hawezi kufanya chochote, nani anatamtunza?

Jamaa ameisambaratisha familia yake yote sasa anaishi peke yake kiasi cha hata yeye mwenyewe ameshaanza kujiona ana matatizo.

Ukiacha Mpakamanga, kuna mwingine yeye hajafukuza watoto wake, ila wamemkimbia kutokana na tabia yake na kushindwa kumudu kuwatunza.

Huyu anapatikana katika wimbo wa DDC Mlimani Park Orchestra, utunzi wake Shaaban Dede, unaitwa, 'Kauli Yako.'

Jamaa amekimbiwa na watoto, amebakiwa na wajukuu ambao kutokana na aina ya maisha ya hapo, huenda nao wakasambaa. Mashairi ya wimbo huu ni haya hapa.

"Kauli yako utoayo mitaani inanifikia nduguyo. Ingawa unafikiri sikufahamu unitetayo sikia, nakuonya uongo mola hauthamini, elewa. Unajitangaza mema mengi kujisifia ya uongo, watoto wamekimbia nyumbani umebaki na wajukuu pia watasambaa.

Iliyobaki nitamwuliza shemeji una kasoro gani hapo nyumbani. Watoto wamekimbia nyumbani umebaki na wajukuu pia watasambaa.

Aaaa. Aaaa, pole mzee. Watoto wanakimbia nini hapo nyumbani. Jirekebishe na hao waliosalia waiondoke. Nitamuuliza shemeji unakasoro gani. Aaaa, Aaaa pole mzee."

Inadaiwa kuwa asili ya Dede kutunga wimbo huu ni dongo kupeleka kwa Juwata Jazz Band, 'Msondo Ngoma.'

Kutokana na Msondo kukimbiwa na wanamuziki wengi ambao walikuwa wakielekea Sikinde, Dede akatupa dongo hilo kuwa inakimbiwa na watoto, na wanamuziki waliojiunga badala yake wakaitwa wajukuu ambao nao baadaye watasambaa.

Licha ya kuwa ni dongo baina na bendi na bendi, lakini maudhui ya wimbo huu yana maana kubwa kwenye maisha ya kawaida kwenye jamii yetu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 13

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

KASSIM alichezewa mchezo na watu wawili, dada na mkewe. Mkewe alijifanya anaondoka akapanga mabegi yake. Dada yake anaangua kilio akidai wifi yake amemtukana matusi ya nguoni yeye na baadhi ya watu wa ukoo wao.

"Kwa nini unalia sasa? Haya si tunayazungumza tu?"

"Nawakumbuka marehemu baba na mama, wamekufa wametuacha mimi na wewe. Wewe ndiyo nakutegemea, lakini naonekana takataka mbele ya mwanamke ambaye amekuja tu, sijui hata ametokea wapi. Amekuja kutufarakanisa mimi na kaka yangu." Havijawa alizidi kutengeneza maigizo.

Kassim alipoona kilio kinazidi akaamua kuondoka kurudi chumbani kwake ambako amemwacha mkewe. Alipoohakikisha kuwa kaka yake ameondoka akanyamaza, akatabasamu na akacheka kicheko cha kebehi.

"Kwenye misiba tu silii nilie kwa ajili hii. Hee! Nitahakikisha anatoka mbwa yule, huu ni mwanzo tu, mwanamke amekuwa kero, kuzaa hazai, kupika hajui, usafi matatizo, hata kujisafisha mwenyewe hawezi, atatoka, mimi siyo Havijawa."

Alipoingia ndani na yeye akatengeneza igizo kwa mkewe.

"Nimempa vipande vyake huko hadi analia."

Mkewe aliposikia hivyo presha ikamshuka, akaanza kuvua nguo zake za safari na kurudisha mabegi yake yalipokuwa awali.

"Ukweli mume wangu kwa hili ni lazima kitu kifanyike. Haiwezekani na hitowezekana tukaendelea kukaa hivi."

"Ni kweli, nimekuwa napata ushauri kutoka kwa watu mbalimbali kuhusu hili, siku chache zijazo nataka kuchukua maamuzi magumu."

**************************************

"Nadhani wewe ndiyo Kassim Kinate, sawa?"

"Ndiyo mimi!"

"Na wewe Havijawa Kinate, si ndiyo dada?"

"Ndiyo!"

"Mimi ni Ofisa kutoka Wizara ya Ardhi, nimekuja hapa kuwaambia kuwa nyaraka za ardhi ya nyumba hii ni feki."

"Nini?" Akauliza Kassim.

"Narudia tena, nyaraka za nyumba hii ni za kughushi. Ofisi yetu imegundua hilo na kwa maana hiyo nyumba yenu ama muibomoe wenyewe au ibomolewe ili mwenye nyaraka halisi achukue eneo lake."

Kassim alionekana kushtuka. Dada yake Havijawa ilikuwa nusura azirai. Hakuamini alichokuwa akikisikia.

"Sisi nyumba hii tumerithi kutoka kwa marehemu baba yetu mzee Kinate Stima."




**"Basi baba yenu alikichukua kiwanja hiki kimakosa, au kinguvu kutoka kwa mtu mwingine. Naye mtu huyo ni marehemu, ila watoto wake walikuja ofisini na kulalamika kuhusu kiwanja hiki. Kuangalia eneo na namba kwenye nyaraka halisi tukaona ni kweli, ila kulikuwa na nyaraka nyingine. Na tulipozikagua tukajidhihirisha kuwa ya marehemu baba yenu ilikuwa feki."**

"Basi baba yenu alikichukua kiwanja hiki kimakosa, au kinguvu kutoka kwa mtu mwingine. Naye mtu huyo ni marehemu, ila watoto wake walikuja ofisini na kulalamika kuhusu kiwanja hiki. Kuangalia eneo na namba kwenye nyaraka halisi tukaona ni kweli, ila kulikuwa na nyaraka nyingine. Na tulipozikagua tukajidhihirisha kuwa ya marehemu baba yenu ilikuwa feki."

"Mtumeee! Sasa tutafanyaje" Akaanza kulalamika Havijawa.

"Kama nilivyosema awali, mbomoe wenyewe ili mtoe vitu vyenu ambavyo mnataka kutoa bila kuharibika, kama matofali, mabati, mbao, madirisha, milango, ili muwaachie wenyewe kiwanja chao, au kwa kuwasaidia mimi kama Ofisa Ardhi ni kwenda kufungua kesi ya kupinga hili ili kesi iendelee na mtafute mwanasheria mzuri ambaye anaweza kuwasimamia."

"Kaka nadhani hilo ndilo tulifanye jamani kama alivyoshauri huku kaka hapa."

"Hapana!" Kassim akaongea kwa sauti ndogo na nzito. Akamshtua dada yake kwa kukataa.

"Siwezi kufanya chochote kwa sasa. Kwa jinsi ninavyoishi kwenye nyumba hii ni kama hainihusu. Ni kama si ya baba yangu. Kwa hili sitolazimika kufanya chochote kwa sababu kufungua kesi na kuweka wakili inahitaji gharama. Na hii gharama nitaibeba mimi mwenyewe. Lakini hapa nyumbani naishi bila raha na mke wangu. Kwa maana hiyo mimi hapa sina mpango napo tena. Nataka niondoke niende sehemu nyingine na mke wangu tukaendelee na maisha yetu."

"Sasa hapa tunamachia nani kaka. Tupambane, hapa ni kwetu!" Havijawa aliongea kwa unyenyekevu uliomshangaza kaka yake Kassim.

"Utabaki wewe! Kama una uwezo wa kuendesha kesi sawa na mimi nakuachia. sitaki kuwa sehemu ya urithi wa nyumba hii, iwe yako peke yako. Mimi nakwenda kuanzisha maisha sehemu nyingine."

"Kaka mimi sina uwezo huo wa kufungua na kuendesha kesi, nakutegemea wewe leo tena unasema unaniachia nyumba, nitaanzaje?"

"Nakuachia, ukishindwa basi, ukishinda ya kwako!"

"Ina maana kaka unashindwa kulitatua hili, unaniachia mimi kweli?" Havijawa akaanza kulia.

"Dada, mimi nimechoka kuishia hapa. Maneno kila siku wewe na wifi yako. Na kwa bahati mabaya hili limetokea, nimeamua kuondoka."

"Sasa wewe unaondokaje unaniacha mimi dada yako?"

"Nakwenda kuishi ukweni! Mke wangu ana baba yake mdogo kule Kibada. Ameshatuambia twende tukaishi kule, yeye haishi pale, ila ana nyumba ambayo ameimaliza, lakini haina mtu wa kuishi."

"Kaka wee, na mimi je nitaenda wapi?" "Havijawa wewe ni mtu mzima sasa, haiwezekani tukafuatana kama watoto wadogo. Mimi nina mke na wewe tafute sehemu ukaishi, ukapange hata chumba." Akajibu Kassim, halafu kama kuna mtu akakumbuka.

"Au nitamuuliza mke wangu kama tunaweza kwenda kuishi wote. Lakini sijui kama atakubali. Hivi mnavyopatana, unafikiri atakubali?" Havijawa hakusema kitu, akabaki analia na moyo wake.

***********************************

Ukweli ni kwamba kile kitu hakikuwa kweli. Hakukuwa na kiwanja feki wala kubomolewa nyumba. Mpango huo ulifanywa na Kassim pamoja na rafiki yake mmoja aitwaye Pembe.

Kwa bahati nzuri, Havijawa alikuwa hajawahi kumwona rafiki huyo wa kaka yake, hivyo alivyokuja pale na kujifanya ni ofisa kutoka Wizara ya Ardhi aliaminika.

Mkakati huu ulitengenezwa ili kuzima tabia mbaya ya Havijawa ya kumnyanyasa wifi yake. Mpaka hapo tayari Havijawa alishajua nyumba itabomolewa, yeye hatokuwa na pa kwenda. Hana mpenzi, hana mume. Hafanyi biashara yoyote. Hajishughulishi ya biashara yoyote ya kumwingizia kipato. Yeye kazi yake kubwa ni umbea tu, kufitinisha watu, pamoja na kumuonea wifi yake.

Aliona kama kaka yake akienda ukweni yeye hawezi kwenda. Anachokifanya kwa wifi yake si kitu ambacho kinaweza kumfanya kukubali wote waongozane wakaishi huko. Kwanza yeye mwenyewe ataanzaje kunyanyua mguu wake, kuongozana na wifi yake kwenda Kibada. Aliona hiyo itakuwa nafasi ya wifi yake kulipiza kisasi.

Siku ya tukio hilo la mpango wa Kassim na Pembe, Sauda hakuwepo. Alikwenda kwao Kondoa kwenye msiba wa ndugu yake. Walijua kabisa mpango huo utamchanganya Havijawa na kweli ilikuwa hivyo.

Wakamwachia mwenyewe sasa kusuka au kunyoa.

Mkutano wa pili ukiwa ni watu wawili tu. Kassim na dada yake Havijawa. Safari hii Kassim alikuwa na wazo moja. Wauze nyumba halafu wagawane pesa nusu kwa nusu, kila mmoja aende anakokufahamu.

"Sasa nyumba si ina kesi hiii kaka, itakuwaje?"

"We hujui mambo ya mjini. Tunamuuzia yeye akiwa hajui, atakaa baadaye wakiwa watu wa ardhi sisi hatupo."

"Mimi naona kama hili si zuri sana, haya tutauza, mimi nitapata pesa, zikiniishia nitakwenda wapi?"

"Sasa hebu niambie dada Havijawa tufanye nini. Mimi naona hii njia ndiyo nzuri kwanza itawafanya wewe na wifi yako msiishi pamoja, maana kila kukicha nyinyi ugomvi tu. Kila mtu akiwa kwake itakuwa safi sana."

Suala hili liliendelea kumchanganya Havijawa. Hakuona kama anaweza kuendesha maisha yake vizuri huko mbele wakiuza nyumba ya baba yao ambayo tayari ina mgogoro.

INAENDELEA JUMAPILI

# KASHFA YA P. DIDDY YAWANASA WENGINE



KASHFA inayomkabili rapa maarufu P Diddy ya unyanyasaji wa kijinsia inazidi kupanuka baada ya msanii mwingine Meek Mill kuhusishwa katika skendo hiyo.

Mapema wiki hii, Rodney "Lil Rod" Jones, mtayarishaji ambaye alifanya kazi kwenye Albamu ya Diddy ya The Love: Off the Grid, alimshtaki Diddy kwa unyanyasaji wa kijinsia.

Hata hivyo, katika sehemu moja ya karatasi za kisheria zinazosambazwa mtandaoni, zinasomeka jinsi Diddy alivyomwambia Jones alivyofanya mapenzi na rapa wa wimbo wa Redacted.


Ingawa majina hayo mawili yalifichwa, inasemekana kuwa kwenye maelezo ya chini yaliyoambatanishwa kwa kila moja, inashukiwa kwamba kesi hiyo inawahusu Meek na Usher kutokana na maelezo husika.

# Fireboy awakosoa wasanii wenzake

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Adedamola Adefolahan maarufu kama Fireboy DML, amesema haufurahii muziki wa Afrobeats nchini humo kutokana na kutokuwa na maudhui ya kiandishi.

Aneawakosoa wasanii wengine wanaofanya muziki huo kwa kushindwa kugusa maisha ya watu wa kawaida na badala yake umekuwa sehemu ya mihemuko ya muda.

Akizungumza na Billboard News, mkali huyo wa kibao cha 'Vibration' amesema 'Tangu mwanzo Afrobeats ilijengewa misingi ya kucheza, hata mimi niligundua kuna kitu kimekosekana, hakuna uandishi, hakuna ushairi, ni kuruka tu, inachosha sana,@ amesema.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JORGINHO ATAKIWA ITALIA

KIUNGO wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho, mwenye umri wa miaka 32 anazivutia Juventus, Lazio na Napoli huku akiingia katika miezi ya mwisho ya mkataba wake. (***Standard***)

### POTTER ATAJWA UNITED

MKURUGENZI wa Michezo anayekuja wa Manchester United, Dan Ashworth, amekutana na aliyekuwa Kocha wa Chelsea na Brighton, Graham Potter, huku shinikizo zikizidi kuongezeka kuhusu Erik ten Hag. (***Sun***)

### ZERBI ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL itamlenga Kocha wa Brighton, Roberto de Zerbi, iwapo watashindwa kumteua Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp anayeondoka. (Guardian)

### KOMPANY KUBAKIA BURNLEY

KLABU ya Burnley inatarajiwa kumbakisha, Vincent Kompany, kama kocha hata kama klabu hiyo itashushwa daraja kutoka kwa Ligi Kuu England. (***Football Insider***)

### MARTINEZ KUTUA BARCA

BARCELONA imewasiliana na Kocha wa Timu ya Taifa ya Ureno, Roberto Martinez, kuhusu kumrithi Xavi kama kocha wa klabu hiyo ya Hispania mwishoni mwa msimu huu. (***Football Transfers***)

### NYOTA VILLA KUUZWA

HUENDA Aston Villa ikalazimika kuuza wachezaji msimu huu wa joto ili kuepuka kukiuka kanuni za faida na uendelevu za Ligi Kuu England, huku Newcastle United ikimtaka kiungo wa kati, Jacob Ramsey, mwenye miaka 22 na Arsenal wanamtaka kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz (25). (***Mail***)

### BROWN AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA, West Ham, Juventus, AC Milan, Nice na Lyon zinavutiwa na mlinzi wa kushoto wa Gent, Archie Brown, mwenye umri wa miaka 21. (***Standard***)

### RAMSDALE ATAKIWA MILAN

AC Milan wanamfuatilia mlinda lango wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Aaron Ramsdale, mwenye umri wa miaka 25, kama mbadala wa mlinda lango wa Ufaransa, Mike Maignan (28). (***Ekrem Konur***)

### ZIDANE AIKATAA ENGLAND

ZINEDINE Zidane hana nia ya kuinoa England kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa wa kukubali ofa yoyote kutoka kwa Manchester United ikiwa watachagua kumwacha, Erik Ten Hag. (***The I***)

### LIVERPOL YAMTAKA ROBERTSON

LIVERPOOL imeonyesha nia na imani kwa beki wa kushoto wa Scotland, Andy Robertson, mwenye umri wa miaka 29, ambaye atabakia katika klabu hiyo msimu huu wa joto licha ya Bayern Munich kumhitaji. (***Football Insider***)

### O'HARE SOKONI ENGLAND

FULHAM, Everton na Southampton zinamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Coventry City mwenye umri wa miaka 25, Callum O'Hare. (***Sun***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# MIKEL AMPELEKA OSIMHEN CHELSEA

**LONDON,** England

## Asema Mnigeria huyo mwenzake ameonyesha nia ya kujiunga...

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, John Obi Mikel, amekiri anaendelea "kutuma ujumbe" kwa Victor Osimhen kuhusu kujiunga na klabu nyingine kutoka Napoli msimu huu wa joto.

Osimhen amekuwa akilengwa na vigogo kadhaa ingawa hivi karibuni alisaini mkataba mpya ambao unajumuisha kifungu cha kutolewa chenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 100 ili kuwezesha kuondoka Napoli msimu wa joto.

Chelsea wanamwania sana mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, lakini Arsenal wanabakia katika kinyang'anyiro cha kuwania saini yake, huku Paris Saint-Germain wakiongeza jina la Osimhen kwenye orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya Kylian Mbappe.

"Nadhani kuna maslahi ya kweli kwa pande zote mbili," alisema Mikel akimwambia, Ben Jacobs, huku akikiri anafanya kama 'wakala'.

**"Nadhani anaipenda klabu. Ni wazi, anataka kufuata nyayo zangu kama mchezaji wa Nigeria am baye amewahi kuichezea Chelsea - Victor Moses na Celestine Babayaro.**

"London jiji la ajabu, badala ya kwenda Liverpool au maeneo megine kuishi London ni sawa kwake. Lakini pia ana maslahi mengi."

"Bado ninasukuma, kumtumia jumbe, nikijaribu kuhakikisha hatarajii mengi, afikirie juu ya klabu moja tu, Chelsea."

Wakati huo huo, Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amekiri hana uwezo wa kumzuia Osimhen kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto kwa sababu ya kifungu chake cha kuachiliwa, ambacho kina thamani ya "kiasi kikubwa sana cha fedha".

"Victor ni mchezaji mwingine mzuri ambaye Napoli wanaye," alisema De Laurentiis akiambia Sky Sports News.

"Tulikuwa na (Edinson) Cavani, (Gonzalo) Higuain, (Ezequiel) Lavezzi na tulikuwa na (Dries) Mertens, tulikuwa na watu wengi ambao walikuwa wazuri.

"Osimhen ni mchezaji mzuri sana - lakini unajua: Napoli ni mahali pazuri. Kuna wachezaji fulani ambao walipenda Napoli na kukaa, kama (Marek) Hamsik kwa miaka 11. Au kama wengine kwa miaka nane. Na kuna wengine ambao wanavutiwa na Real Madrid, PSG, Arsenal, Manchester City, Chelsea.

"Kwa hiyo huwezi kuwazuia, haswa wanapokuwa na kiwango maalum cha fedha ambacho wanaweza kununuliwa."

HABARI MICHEZO

# ROBERTSON ATAJWA KUMRITHI DAVIES




**MUNICH,** Ujerumani

MLINZI wa Liverpool, Andy Robertson, ni mmoja wa mastaa wanaowindwa na Bayern Munich katika dirisha lijalo la majira ya joto ili akazibe nafasi ya Alphonso Davies, anayedaiwa yupo kwenye hatua za mwisho za kujiunga na Real Madrid.

Vigogo wa Bayern Munich wanaamini itakuwa kazi ngumu kuipata saini ya Robertson mwenye umri wa miaka 29 mwisho wa msimu huu, lakini wanataka kupambana kuhakikisha wanamsajili.

Beki huyo anatarajiwa kutimiza umri wa miaka 30, mwezi ujao lakini licha ya umri wake bado anaonekana ni mmoja kati ya wachezaji bora kwenye kikosi cha Liverpool na Ligi Kuu England, jambo linalowapa matumaini Bayern Munich kuamini anaweza kwenda kuziba pengo la Davies.

Hadi sasa Robertson, amecheza mechi 280 za michuano yote na ameshinda mataji yote makubwa. Kwa sasa beki huyo amebakisha miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2026.

Katika msimu huu amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara yaliyosababisha acheze mechi 15 za michuano yote.

# Benitez afunguka kuhusu Alonso

**MADRID,** Hispania

RAFA Benitez amemtaka, Xabi Alonso, kutoharakisha hatua nyingine ya maisha yake ya soka bali ajiunge na timu ya juu mara tu atakapajihakikisha yuko tayari.

Alonso, ambaye alicheza chini ya Benitez katika klabu ya Liverpool, ameushambulia ulimwengu kwa kasi akiwa na Bayer Leverkusen na ndiye anayelengwa na Wekundu hao na Bayern Munich.

Licha ya kutamani sana huduma yake, Alonso pia amependekezwa kung'ang'ania Leverkusen kwa angalau msimu mmoja zaidi, na Benitez alikiri kufanya hivyo inaweza kuwa hatua nzuri katika taaluma yake ya ukocha.

"Kwa mitandao ya kijamii kila kitu kinakwenda haraka sana," alisema Benitez, ambaye aliiongoza Liverpool kati ya mwaka 2004 hadi 2010, akiliambia The Times.


"Naweza kuelewa kwa nini Alonso anapigiwa debe, kwa sababu anafanya vizuri sana na Leverkusen na ni jina kubwa, mtaalamu mzuri, kijana mzuri, mwerevu... lakini fikiria (Steven) Gerrard anaweza kuwa karibu na kufanya vizuri. Basi itakuwa 'Gerrard!'.

"Ana uwezo wa kuwa kocha mzuri sana na ikiwa ana wachezaji wazuri atafanikiwa, lakini anaweza kufanya hivyo kwa miaka mitano, miaka 10? Sijui.

"Anaweza kwenda upande wowote wa juu sasa, lakini wanatarajia kushinda taji. Na ukimaliza wa pili, labda ni msimu mzuri lakini watu watasema, 'Ameshindwa.



# Dier kimeeleweka Bayern Munich



**MUNICH,** Ujerumani

ERIC Dier atajiunga na Bayern Munich kwa uhamisho wa kudumu msimu huu wa joto baada ya mkataba wake wa mkopo kutoka Tottenham Hotspur kumalizika, kwa mujibu wa ESPN.

Dier alijiunga kwa uhamisho wa mkopo wakati wa dirisha la uhamisho wa Januari na amekuwa akianza mara kwa mara chini ya Kocha, Thomas Tuchel, akianza michezo minne kati ya sita ya Bundesliga hadi sasa.

Mkataba wake na Bayern Munich ulipaswa kudumu kwa miezi sita, muda sawa na mkataba wake wa Tottenham - lakini ulijumuisha kipengele ambacho kinaweza kumfanya akae Munich na kuongezwa kwa miezi 12 zaidi.

Kwa mujibu wa Fabrizio Romano, Dier alihitaji kucheza mechi tatu pekee kabla ya mkataba wa mkopo, ambao Bayern Munich walilipa takriban euro milioni nne, ungefanywa wa kudumu.

Wakati gazeti la The Athletic likiripoti kikosi cha Ujerumani kimefurahishwa na matokeo yake tangu alipojiunga Januari, mwaka huu, Bild hivi majuzi ilisema kulikuwa na wasiwasi juu ya utimamu wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Maswali kuhusu kutokuwa na kasi yake yamesababisha kuendelea kwa Dier na Bayern Munich kuibuliwa mjadala, lakini bila kujali msimamo wao, Bayern Munich sasa itabidi waje na mpango wa beki huyo mahiri kabla ya msimu ujao.

Dier anaonekana kuaminiwa na Tuchel, lakini atalazimika kujiaminisha kwa kocha mpya msimu ujao kwani Bayern Munich tayari wamethibitisha watabadilisha bosi wao mwishoni mwa msimu huu.

## Kidunda amtaka tena Wellem

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa Tanzania, Selemani Kidunda, amesema ameumizwa na matokeo ya sare aliyoyapata na anataka pambano la marudiano dhidi ya Asemahle Wellem, raia wa Afrika Kusini ili athibitishe ubora wake.



Pambano hilo la raundi 12 la uzito wa kilo 76 la kuwania mkanda wa WBF lililofanyika kwenye ukumbi wa Warehouse, Dar es Salaam, linakuwa ni sare ya pili kwa Kidunda tangu alipoanza kucheza ngumi za kulipwa.

Akizungumza na Nipashe baada ya pambano hilo, Kidunda alisema Wellem ni mpinzani ni mzuri lakini sare aliyopata imemuuma na 'imechafua' rekodi zake jambo ambalo hakutarajia litokee.

"Siwezi kuwapinga majaji wameamua, mimi kama Selemani Kidunda naomba nirudiane naye tena mechi nyingine, sina mengi ya kusema nawashukuru Watanzania wote walionisapoti," alisema Kidunda.

Naye Wellem alisema lilikuwa pambano zuri na tangu ajiunge na ngumi za kulipwa alikuwa hajawahi kuangushwa ulingoni ingawa alifanikiwa kunyanyuka mapema na kuendelea.

"Katika mapambano saba niliyocheza kwenye ngumi za kulipwa hii ni mara yangu ya kwanza kuangushwa ulingoni, lakini nikaamka mapema, tunaendelea kukua na kujifunza mambo mengi, nahitaji pambano la marudiano na nitakapomwangusha asiamke tena," alisema Wellem.

Katika pambano lingine, Nasib Ramadhani aliibuka mshindi dhidi ya Emmanuel Naidjala kutoka Namibia kwa pointi 80-71, 80-72 huku jaji mmoja akitoa sare ya 79-79 wakati Salim Mtango alimdunda Mmalawi, Grey Chikwapulo.

# MBEYA CITY YAWAZUIA PAMBA KUKAA KILELENI

**Na Adam Fungamwangwo**

IKIWA nyumbani, Pamba FC imeshindwa kutamba baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Mbeya Kwanza katika mechi ya raundi ya 23 ya Ligi ya Championship iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza juzi.

Pamba ilihitaji ushindi wa aina yoyote ili kufikisha pointi 51, na kuwapiku vinara wa ligi hiyo, KenGold wenye pointi 50.

Matokeo hayo yamewafanya Pamba kubakia katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo wakifuatiwa na Mbeya Kwanza ambayo imefikisha pointi 46.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, Mbeya City, ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya, ililazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Stand United kutoka Shinyanga.

Mabao ya Mbeya City katika mechi hiyo yalifungwa na Maulid Shaaban na Pius Joseph, huku yale ya Stand United yakiwekwa kimiani na Lucas Sendema na Mtikila Hussein.

Wakati huo huo, golikipa wa KenGold, Castor Mhagama, anaongoza kwa kukaa mechi nyingi bila kuruhusu nyavu zake kutingishwa maarufu 'clean sheets.'

Kipa huyo amekaa langoni mechi 14 bila kuruhusu nyavu zake na kuguswa na wapinzani katika ligi hiyo.

Mhagama anaifanya KenGold kuongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 50 mpaka sasa.

Anafuatiwa wa kipa wa TMA, Yusuph Abdul, ambaye ana 'clean sheets' 12, huku nafasi ya tatu inachukuliwa na kipa mkongwe aliyewahi kuichezea Azam FC, David Kissu ambaye ana amekaa langoni mara tisa bila wavu wake kuguswa, wakati kipa wa zamani wa Simba ambaye kwa sasa anaichezea Mbeya City, Jeremiah Kisubi, ana 'clean sheets' nane.

Wengine ni Adam Oseja wa Cosmopolitan mwenye 'clean sheets', Christopher John wa JKT Tanzania, Fahad Idrisa wa Green Warriors ambao wana 'clean sheets' sita kila mmoja.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), wakifanya mazoezi kujiandaa na Michezo ya Afrika (All Africa Games), itakayofanyika Accra, Ghana baadaye mwezi huu. **PICHA: TFF**

# Ngome FC yatamba haishuki daraja

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

LICHA ya kupata matokeo mabaya, Kocha Mkuu wa Ngome FC, Omar Khamis 'Matu' amesema bado anaendelea na mipango ya kuijenga timu yake ili kuhakikisha inabakia katika Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu mwingine mpya.

Ngome FC imepanda daraja msimu uliopita na ni moja ya timu ambazo zimefanya vibaya katika mechi za Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea ambayo huyoa mwakilishi wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ngome FC katika michezo 20 waliyocheza wameshinda mechi tatu, wamefungwa michezo 10 na wametoka sare michezo saba, na matokeo hayo yanawafanya kukaa katika nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye msimamo wa ligi hiyo waki na pointi 16 kibindoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matu alisema ameanza kupata matumaini ya kubakia katika ligi hiyo kutokana na mwenendo wa kiuchezaji uliobadilika kwa wachezaji wake kwenye michezo mitano iliyopita.

Matu alisema kwa sasa wachezaji wake wameimarika na kila mmoja yuko tayari kupambana kuhakikisha wanatimiza malengo ya kubakia katika Ligi Kuu Zanzibar.

"Kwa sasa kikosi changu kimebadilika, wachezaji wanacheza vizuri na hii inaonyesha wanahitaji kupata matokeo chanya katika michezo wanayocheza bila kujali ugumu wa timu wanayokutana nayo," alisema Matu.

Kocha huyo aliongeza ligi ni ngumu lakini wachezaji wake wanasema hawajakata tamaa na sasa kila mechi kwao itakuwa ni sawa na fainali na si vinginevyo.

"Wachezaji wangi wananipa matumaini makubwa katika kuhakikisha tunapata ushindi, tunapambana ili kuibakisha timu katika Ligi Kuu, kwa sababu hata timu zilizopo juu yetu tumepishana alama mbili tu, hakuna kisichowezekana," Matu alisema.

Aliongeza mipango iliyopo katika timu yake ni kuhakikisha michezo saba iliyobakia wanapata ushindi na hapo watafikisha malengo waliyonayo.

"Tumecheza michezo 20, tuna michezo 10 mikononi, hivyo michezo hii huenda tukacheza baada ya mwezi wa Ramadhani, ni lazima tuhakikishe tunafanikiwa walau kushinda michezo sita na kufanikisha malengo yetu," alisema kocha huyo.

Aliwaomba mashabiki wa timu hiyo yenye makazi yake eneo la Fuoni kuendelea kuwapa hamasa wachezaji wao ili kuipigania kusaka matokeo mazuri kwa kujitokeza kwa wingi kushangilia wanapokuwa na mechi jirani.

Michezo
Jumapili Machi 3, 2024
Nipashe



Mikel ampeleka Osimhen Chelsea UKU. 21

# THIS IS SIMBAAA

## ●●● Yatinga robo fainali CAF kibabe, yalipa kisasi, Chama utampenda...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO sita yaliyofungwa na wachezaji tofauti yaliiwezesha Simba kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya nne, huku ikifanya hivyo mara mbili mfululizo katika michuano hiyo.

Wachezaji waliopachika mabao hayo ni Mrundi Saido Ntibazonkiza, Pa Omari Jobe kutoka Gabon, Mzambia Clatous Chama, Mkongomani, Fabrice Ngoma na Watanzania wawili, Kibu Denis na Ladaki Chasambi.


Simba, ikiwa kwenye uwanja wa nyumbani, Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ilipata ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy na pia kulipa kisasi cha Oktoba 24, 2021 ilipofungwa klabu hiyo ya Botswana magoli 3-1 na kutolewa katika hatua ya makundi.

Ushindi huo wa Simba unaifanya Tanzania kwa mara ya kwanza kuingiza timu mbili katika hatua ya robo fainali, baada ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Yanga kutinga hatua hiyo mapema baada ya kuitandika CR Belouizdad mabao 4-0, mechi iliyochezwa Februari 24, mwaka huu hapa nchini.

Tanzania inakuwa nchi pekee msimu huu kuingiza timu mbili katika hatua hiyo, huku zilizobaki zikiwa na timu moja tu.

Alikuwa ni Saido aliyeanza kuwanyanyua vitini mashabiki wa Simba alipopachika bao la kwanza dakika ya saba ya mchezo.

Mpira ulianzia kwa Chama ambaye aliwapepeta mabeki wa Jwaneng Galaxy, na kupiga krosi, lakini ikaokolewa na Moagi Sechele, ambaye alichotaka kukifanya hakikuwa na mpira huo ulimrudia Mzambia huyo aliyemwona mfungaji akiwa sehemu nzuri, kabla ya kumpa pasi ya upendo, mpira ukajazwa wavuni kwa mguu wa kulia.



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kushoto), akijiandaa kupiga shuti katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 6-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

Dakika nane baadaye, straika aliyesajiliwa kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo, Jobe, aliandika bao la pili, baada ya kupokea krosi safi kutoka kwa Saido.

Kabumbu ilianza kwa Kapombe, aliyekuwa wingi ya kulia, akaupiga ndani kwa Chama ambaye aliupiga juu ukipita vichwa kwa mabeki wa Jwaneng na kumfikia Saido aliyefanya kazi ya kumwekea mfungaji, aliyemalizia kuusukuma wavuni kirahisi. Chama, alihusika kwa mara nyingine tena katika bao la tatu, alipoambaa na mpira wingi ya kushoto na kuingiza majaro yaliyozua kizaazaa langoni kwa wageni hao, kabla ya Kibu kuukwamisha wavuni dakika ya 22.

Simba ingeweza kwenda mapumziko ikiongoza kwa mabao 5-0 kama mashuti mawili ya Chama yasingegonga nguzo ya chini ya upande wa kulia dakika ya 38 na 41, mara zote hizo, aliwatoka mabeki wa Jwaneng Galaxy na kubaki ana kwa ana na kipa.

Kipindi cha pili, wachezaji wa Jwaneng Galaxy wakaamua kucheza mchezo wa kuotea, wakiaacha wachezaji wa Simba peke yao na kila wanapopigia mpira wanajikuta 'wamejenga vibanda.'

Shambulizi pekee la hatari kwa Jwaneng Galaxy lilifanywa dakika ya 71, wakati straika wao aliyekuwa akijitutumua kwenye mechi hiyo, Thabang Sesinyi, alipowatoka mabeki wa Simba na kubaki na Ayoub Lakred, lakini shuti lake lilitoka nje.

Chama alirekebisha makosa yake dakika ya 75, alipopachika bao la nne, kwa shuti la mbali, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Kibu kuuzuia mpira uliopigwa na kipa, Phoko, akaupeleka kwa Ngoma, aliyempa Saido, akaumwekea kiungo huyo ambaye jana alikuwa 'moto' na kuukwamisha wavuni.

Ni kama Simba walishatambua jinsi ya kuutegua mchezo wao wa kuotea, kwani walipeleka mashambulizi mfululizo mwishoni mwa mchezo na dakika nne kabla ya mechi kumalizika, mchezaji chipukizi, Ladaki Chasambi akaukwamisha mpira wavuni uliokuwa umetemwa na kipa, Phoko ambaye alipangua shuti la Freddy Michael.

Chasambi na Freddy wote waliingia kipindi cha pili. Kama vile haitoshi, Ngoma akapigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Jwaneng Galaxy, alipofunga bao pekee la kichwa kwenye mchezo huo.

Simba imemaliza mechi zake za Kundi B, ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi tisa kama ilivyokuwa na Wydad Casablanca ya Morocco, ambayo jana nayo ilishinda nyumbani bao 1-0 dhidi ya Asec Mimosas.

Hata hivyo, Wekundu wa Msimbazi wananufaika na matokeo ya timu hizo mbili zilipokutana Simba ikifungwa bao 1-0 ugenini na kushinda 2-0 nyumbani, hivyo matokeo ya jumla kuwa mbele kwa mabao 2-1.

# Yanga yazipigia hesabu pointi 12

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupoteza mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini dhidi ya Al Ahly ya Misri, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema sasa mawazo yake anayaelekeza kwenye Ligi Kuu Bara kwa kuzitaka pointi 12 za michezo minne inayofuata ya ligi hiyo ya juu nchini.

Yanga imemaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi D ikiwa na pointi nane nyuma ya vinara Al Ahly waliofikisha pointi 12 baada ya ushindi wa bao 1-0 katika mechi iliyowakutanisha juzi.

Katika Ligi Kuu Tanzania Bara, mabingwa watetezi, Yanga watakuwa ugenini dhidi ya Namungo FC Machi 8, mwaka huu na siku tatu baadaye watawakaribisha Ihefu FC na michezo yake inayofuata itakuwa ni dhidi ya Geita Gold FC na Azam FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema mechi yao dhidi ya Al Ahly ilikuwa ya ushindani mkubwa na anawapongeza wachezaji kwa kucheza vizuri ingawa bahati ya ushindi haikuwa upande wao.

Gamondi alisema nyota wake walionyesha kiwango kizuri na baada ya kumaliza mechi hiyo, wanarudi kujiandaa na kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza ili kujiweka sawa kuondoka na ushindi katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara lakini pia kujipanga na hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tulipata nafasi tukashindwa kuzitumia kwa sababu ya kukosa umakini, tunarejea nyumbani kusahihisha makosa yetu na kuanza kujiandaa na hatua inayofuata, lakini kwanza tunaangalia kilichopo mbele yetu ni michezo ya Ligi Kuu," alisema Gamondi.

Aliongeza Al Ahly wametumia vizuri nafasi waliyopata na mechi hiyo imewaongezea mbinu katika maandalizi ya michezo ijayo ya Ligi Kuu Bara na ule wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Naye Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema kikosi cha timu hiyo kilirejea nchini jana na kuanza maandalizi ya kuwakabili Namungo.

"Tuna mechi nne za ligi na tunahitaji kupata matokeo chanya katika mechi hizo, ligi itakuwa katika mapumziko kupisha kalenda ya FIFA na baada ya hapo tutakuwa na maandalizi yetu ya kujiandaa mchezo wa robo fainali," alisema Walter.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >